SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Viongozi** wa dini wamwombea Rais Samia

UKURASA 4




UKURASA 20

Jumapili Januari 30, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580841
www.ippmedia.com
w.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Masauni, polisi kujadili mauaji

• **Kujifungia** kutafuta mbinu za kuyadhibiti, mwingine auawa madai ya kutengeneza radi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MABADILIKO MAKUBWA KATIKA SERA YA ELIMU**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imezindua mpango mkakati wa kitaifa wa miaka mitano wa elimu...

**UKURASA WA 3**

**MSAJILI AIPA KONGOLE ACT- WAZALENDO**

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, amevitaka vyama vya siasa kuiga Chama cha ACT-Wazalendo...

## Shein aonya viongozi CCM utendaji kazi kwa mazoea

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe Mama Mbonimpaye Mpango, wakimsikiliza mwongoza watalii, Mzee Kassim Mbingo, kuhusu vyombo vya asili vya kuhifadhia chakula na maji vya wakazi wa Kigoma, vilivyopo katika makumbusho ya kihistoria ya Dk. Livingstone, Ujiji mkoani humo jana. **PICHA: OMR**

## Msako kila nyumba wanafunzi walioshindwa kwenda sekondari

UKURASA 2

**MICHEZO** **MAYELE AIPELEKA YANGA 16 BORA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Masauni, vigogo polisi kujifungia kutafuta mbinu kudhibiti mauaji

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na mauaji yanayoendelea nchini, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni amepanga kukutana na Watendaji Wakuu wa Jeshi la Polisi ili kujadili jinsi ya kudhibiti mauaji hayo.

Waziri Masauni amesema katika kikao hicho pia watajadili jinsi ya kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa katika kudhibiti matukio mbalimbali kiuhalifu nchini.

Akizungumza katika ziara yake ya siku moja ya kutembelea Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi (Forensic Bureua) jijini Dar es Salaam jana, Masauni alisema lengo kuu la kukutana na viongozi hao kesho ni kupata taarifa ya uchunguzi wa mauaji na kujua jinsi gani matukio hayo yanaweza kumalizwa katika jamii.

"Jumatatu (kesho) nitakuwa na kikao na viongozi wa Jeshi la Polisi wakiongozwa na Mkuu wa Jeshi, IGP Simon Sirro wizarani kwa ajili ya kupitia matokeo ya kazi ya uchunguzi ambayo wanaifanya. Serikali tunategemea waifanye ili kuwajulisha wananchi juu ya hayo matukio yote ili tujue tulipofikia, hatua zake ni zipi, na mafanikio yake ni yapi na mikakati kuweza kuhakikisha mambo kama haya ya mauaji tunaweza tukayapunguza katika siku za usoni," alisema Masauni.

Waziri Masauni aliongeza kuwa lengo la ziara yake ni kutaka kuona kamisheni hiyo ya uchunguzi inavyochunguza na kudhibiti mauaji pamoja na kuhakikisha wahalifu wanapatikana kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Masauni alizungumzia kuhusu uhalifu wa kimtandao na kuliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka wanaosajilia watu laini za simu, wanaochafua viongozi na wanaosambaza picha chafu mitandaoni.

Suala la uhalifu wa kimtandao, alisema limekuwa kubwa katika siku za karibuni na kadiri siku zinavyokwenda na teknolojia inavyozidi kutanuka ndipo matatizo ya uhalifu wa kimtandao yanavyoongezeka.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni lazima jeshi liwe tayari kukabiliana na mabadiliko ya aina yoyote katika kudhibiti uhalifu huo ambao haukubaliki na hauwezi kuachwa uendelee.

"Wako watu wamekuwa wakitumia mitandao vibaya kudhalilisha watu wengine. Wengine ni watu wazima wanaweza kuwa hata wazazi wao. Wako wanaotumia mitandao kufanya wizi na kutapeli raia wengine na wako watu ambao wanajadili mambo ambayo ni kinyume cha maadili na desturi za Watanzania.

"Haya yote yanayoendelea kufanyika lazima yadhibitiwe na Jeshi la Polisi. Kwa hiyo kuna haja ya kuhakikisha haya yote yanafanyika kwa kasi zaidi," alisema Masauni.

Mkuu wa Kitengo cha Uhalifu wa Kimtandao, Mrakibu Mwandamizi Joshua Mwangasa, alimshukuru waziri huyo kwa kutembelea Kamisheni hiyo na kuahidi kutekeleza maelekezo yote aliyoyatoa.

"Namuahidi Mheshimiwa Waziri na serikali kwa ujumla hili suala tutalifanyia kazi usiku na mchana. Amejionea mwenyewe tunavyofanya kazi na jinsi gani tunavyopambana na uhalifu wa kimtandao. Kwa hiyo cha msingi ni kupokea maelekezo na kuyafanyia kazi ili changamoto nyingi sana tuweze kuzifanyia kazi na kuzimaliza," alisema SSP Mwangasa.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (katikati), akizoa takataka aliposhiriki katika zoezi la usafi katika Kata ya Manzese jana, ambalo hufanyika kila mwisho wa mwezi mkoani humo. **PICHA: MAULID MMBAGA**

## Auawa kwa tuhuma za kutengeneza radi

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MTU mmoja ameuawa na wananchi kwa tuhuma za kishirikina akidaiwa kuwa anatengeneza radi kwa ajili ya kuua watu.

Hatua hiyo imetokea baada ya mvua iliyonyesha Januari 24, mwaka huu katika kijiji cha Mtisi Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi iliyoambatana na radi iliyompiga Angelina Revocatus (16) na kufariki dunia akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa mjini hapa.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Sylvester Ibrahim, alimtaja aliyeuawa kwa madai hayo kuwa ni Baraka Said (30) mkazi wa Mtisi, Kamanda Ibrahim alisema Said alipigwa na kitu kizito kichwani na kukatwa na kitu chenye ncha kali kwenye paji lake la uso.

Alisema mpaka sasa watuhumiwa wanane wamekamatwa kuhusiana na tukio hilo. Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni John Mayonjuwa, Mashaka Mathias, Sele Richard, Revocatus Raymond, Julius Dalali, Hawa Rashidi, Agnes Rashid na Tausi Abdul.

Ibrahim alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani mara baada ya upelelezi kukamilika.

Kamanda Ibrahim aliwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi vitendo vinavyosababisha matukio ya kujeruhi watu na mauaji pia.

# Msako kila nyumba wanafunzi walioshindwa kwenda sekondari

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ametangaza msako wa nyumba kwa nyumba kuanzia kesho kwa wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni.

Amesema kwa wanafunzi watakaokamatwa adhabu watakayopewa wazazi ni kudeki vyoo vya walimu.

Mtaka aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wazazi, walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Zuzu ambayo kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka jana, ilishika nafasi ya 51 kati ya 52 mkoani Dodoma.

Alisema msako huo utafanywa kwa kutumia mgambo na kwamba kwa mzazi ambaye atakuwa hajampeleka shuleni mtoto atapewa adhabu ya kufanya usafi kwenye shule ikiwamo kudeki vyoo.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka watendaji wa mitaa kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, wanafika shuleni haraka ili kuanza masomo.

Alisema kwa wazazi ambao wanadai wamewapeleka watoto wao shule binafsi, simu zitapigwa shule husika ili kuhakiki kama ni kweli au laa.

"Nasema hili sitanii nitalisimamia kwa nguvu zote sitaki kusikia mtoto anabaki nyumbani nataka aje shule, kwangu mtaelewa kwa nguvu na hapa ninamanisha sina utani katika hili. Nitahakikisha mpaka mnakimbia nyumba zenu sitaki utani katika hili," alisema.

Mtaka aliwataka wazazi kuwasaidia watoto wao kutimiza ndoto za kusoma na kuacha kulalamika kwamba wanatembea umbali mrefu.

"Kila mzazi abebe hasira za kuhakikisha mtoto wake anasoma na kufaulu, ajenda ya elimu iwe kipaumbele kwa kila mmoja sitaki kusikia habari ya maneno maneno wanafunzi wanatakiwa kusoma," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Dismas Chilala, alisema wanakabiliwa na tatizo la uelewa wa wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa elimu.

Diwani wa Zuzu, Awadh Abdallah, alisema kumekuwapo na tatizo la wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuchukuliwa na kwenda kufanya kazi za ndani.

Mmoja wa wazazi, Ernest Chisota, alisema tatizo kubwa linalowakabili kwenye shule hiyo ni ukosefu wa maabara pamoja na baadhi ya walimu kutoingia darasani.

## HABARI KITAIFA

# Naibu Msajili aipa kongole ACT-Wazalendo

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, amevitaka vyama vya siasa kuiga Chama cha ACT-Wazalendo kwa kufanya uchaguzi unaofuata demokrasia.

Amesema ACT-Wazalendo kimefuata misingi na taratibu sahihi za demokrasia kwa kuandaa mfumo mzuri wa kuwapata viongozi ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi ndani ya chama hicho.

Aliyasema hayo jana wakati wa Mkutano Mkuu Maalumu wa chama hicho uliofanyika mkoani Dar es Salaam, uliokuwa na lengo la kufanya uchaguzi wa viongozi wa ngazi za juu.

Viongozi hao ni Mwenyekiti wa ACT -Wazalendo Taifa, ambaye atakuwa mrithi wa Hayati Maalim Seif Sharif Hamadi, nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar pamoja na mjumbe mmoja wa Halmashauri Kuu.

Akihutubia katika mkutano huo, Nyahoza, aliipongeza ACT-Wazalendo kwa kufuata misingi na taratibu sahihi ya demokrasia kwa kuandaa mfumo mzuri wa kuwapata viongozi hao.

Nyahoza alisema mfumo unaotumiwa na chama hicho ni wa ushindani, ustaarabu kwa watu kugombea katika nafasi mbalimbali.

"Tunawapongeza kwa kuandaa mkutano huu, nimehudhuria mikutano mingi ya vyama vya siasa huu umepangwa vizuri. Kuandaa mkutano mkuu siyo jambo dogo, pia tunawapongeza kwa kuheshimu na kutekeleza matakwa ya kidemokrasia kwa sababu tunaelewa tulipata tatizo kubwa kama nchi la kuondokewa na Hayati Maalim Seif Sharifu Hamad," alisema Nyahoza.

Aidha, alitoa wito kwa vyama vingine vya siasa kuiga mfumo huo na kuweza kuboresha suala la demokrasia, akisema kwamba bado kuna changamoto ya demokrasia katika vyama vya siasa.

"ACT-Wazalendo ni kati ya vyama ambavyo vina ukomavu mkubwa wa kisiasa, mnafanya siasa ya kistaarabu, mmetoka kwenye uchaguzi pamoja na changamoto za wakati ule lakini mkaingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tuliandaa mkutano wa wadau pale Dodoma mlishiriki ule ni ukomavu wa kisiasa," alisema Nyahoza.

Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe aliwashukuru wanachama wa chama hicho wa ndani na nje ya nchi kwa michango yao iliyowezesha suala hilo kukamilika, akidai kuwa bila ushirikiano wao mkutano huo usingefanikiwa.

Alisema licha ya madhila waliyokutana nayo nyakati za nyuma lakini waliamua kusimama imara na kuwa na umoja ambao umewawezesha kufika walipo sasa. Zitto alisema: "Wakati tunajenga chama ni lazima tuendeleze agenda za kitaifa, kwetu sisi tunajenga chama wakati tunapambania mabadiliko ya kisheria na kisiasa, tunatambua umuhimu wa katiba mpya.

"Tuhakikishe uchaguzi unaofuata uwe na tume huru ya uchaguzi, sisi ni lazima tuwe na kila aina ya mbinu, tutaheshimu sheria za haki lakini hatutaheshimu sheria ambazo zinaminya haki za watu." alisema



Vijana wa halaiki wakitumbuiza na picha za viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiwemo waasisi wa Taifa, wakati wa ufunguzi wa sherehe za maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa CCM, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Dk. Shein akemea utendaji wa mazoea

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wanachama na viongozi wa serikali, kubadili utendaji kazi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kujenga utamaduni wa kuwa wamoja na wenye kujali maslahi ya nchi.

Dk. Shein aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 45 ya CCM yaliyofanyika katika uwanja wa Mwehe, Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema akiwa Rais alijaribu kuwaasa wananchi kuacha kufanya kazi kwa mazoea katika serikali na sekta binafsi kwa kutambua umuhimu wa kutekeleza ilani ya uchaguzi inayoendelea kufanyiwa kazi ikiwamo kuendeleza sera ya uchumi wa bluu.

Sera ya uchumi wa bluu, alisema ni ya CCM na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amekuwa akisisitiza utekelezaji wa ilani ya uchaguzi. Alisema Dk. Mwinyi anahitaji kupewa pongezi kwa kuwa amewawezesha kutafuta wataalamu ambao wana uwezo wa kutoa taaluma zao kwa kushauriana na serikali katika sekta zote za uchumi na maendeleo na jamii.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, CCM inaadhimisha siku hiyo ikiwa bado iko madhubuti na imara na imepata mafanikio makubwa na baadhi ya vyama vilivyoundwa vimekufa na vingine vimeyumba.

Pia alisema viongozi na wana CCM kuhakikisha wanaitekeleza vyema ilani ya uchaguzi ili kukifanya chama kushinda katika uchaguzi mkuu ujao Bara na Visiwani.

"Wanachama wa CCM waisome historia ya CCM kujua kwa nini inaaminika kuendeleza dola, kwa uwazi, kwani chama hakimwangalii mwanachama alivyo, ila kimekuwa na utaratibu wa uwazi ambao unaanzia kwenye shina jambo ambalo linatufanya kupata viongozi bora" alisema Dk. Shein.

Alisema mfumo wa vyama vingi ulikubaliwa na CCM na umesaidia kuleta ushujaa mkubwa na kuaminiwa na wananchi.

Alisema programu zinazoandaliwa na CCM zina dhamira ya kuwawekea malengo mazuri wananchi na ndio maana kimekuwa na uwezo mkubwa wa kusimamia mambo yake.

Pia alisema kasi ya kujitolea imepungua na inahitaji kuangaliwa upya kwa kuwa hakuna hasara itakayopatikana kwa vile nchi nyingi duniani bado zinafuata mfumo huo.

Aidha, alisema ilani ya mwaka 2020 imeanza kutekelezwa vizuri jambo ambalo limeonyesha mafanikio baada ya sekretarieti kujiridhisha katika ziara zake.

Dk. Shein alisema kuna haja kwa wanachama wa CCM kuangalia walipotoka na wanapokwenda kwa kuhakikisha wanaitunza historia hiyo, ili ifanye vizuri zaidi na vizazi vijavyo viweze kufaidika nayo.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema CCM imeendelea kuaminiwa na Watanzania kushika dola kwa kupewa kura nyingi huku kukiwa na mafanikio mbali mbali yaliyofanyika katika sekta mbali mbali ikiwa ni pamoja na kulinda na kudumisha uhuru wa Tanzania ikiwemo tunu ya Amani na utulivu.

Alisema uzinduzi wa kadi za kielektroniki unatarajiwa kufanyika Febuari 5, mwaka huu, ikiwa ni hatua itakayoimarisha vyema mtandao wa chama hicho.

Chongolo alisema chama kilitoa mwongozo wa kuruhusu kujikosoa katika vikao vya ndani ambapo ulisaidia kuwapa nafasi ya kukosoana bila kuwapo mivutano.

Alisema mradi wa awamu ya nne wa chama hicho utakuwa kuongeza wanachama, kutoa kadi za kielektroniki zitakazokuwa za kudumu pamoja na kusimamia rasilimali za chama, kuimarisha huduma katika mashina na matawi, kukuza demokrasia na kudumisha Mapinduzi ya mwaka 1964 na kuviimarisha vyombo vya habari vya chama hicho.

# Mabadiliko makubwa katika sera ya elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imezindua mpango mkakati wa kitaifa wa miaka mitano wa elimu jumuishi, huku ikitaja mambo matano yatakayotekelezwa ikiwamo kurekebisha sera ya elimu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Eliamini Sedoyeka, aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua mkakati huo wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, jijini hapa.

Prof. Sedokeya alisema katika maeneo ya utekelezaji wa mkakati huo sera ya elimu itarekebishwa ili iendane na elimu jumuishi katika ngazi zote za elimu, ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Alitaja eneo lingine ni kuimarisha upatikanaji wa elimu bora na kwa usawa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwenye ngazi zote za elimu.

Pia, alitaja eneo la tatu ni kuwajengea uwezo watunga sera, wafanya maamuzi, watekelezaji na jamii kuhusu umuhimu wa elimu jumuishi kwa ngazi zote na wadau ili kurahisisha ufanyaji tathmini.

Aidha, alisisitiza mpango huo utalenga kuwa na mfumo wa elimu unaotoa fursa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupata elimu bila vikwazo, mazingira, kiuchumi na kitaasisi katika ngazi zote. Mkurugenzi wa Elimu Maalumu na Jumuishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya alisema mpango mkakati huo umeboreshwa na utaendana na mahitaji ya sasa.

Kamishna wa Elimu nchini Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema kuzinduliwa kwa mkakati huo ni lengo la kumwezesha kila mtoto wa kitanzania anapata elimu bora na kwa usawa kwa maendeleo ya Taifa na jamii kwa ujumla.


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…………………….. 2021**
**In the matter of the Estate of the late CHIPANHA MWANANGOTO KUTAMIKA of NG'HONG'HONHA Area within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOYCE NDAHANI BODE**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 31/01/2022.

**Dated at Dodoma this 11TH day of November 2021**

…………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

# Viongozi wa dini wamwombea Samia

**Na Mary Geofrey**

VIONGOZI wa dini nchini, jana walikutana kwa ajili ya kusherehekea miaka 62 ya kuzaliwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na kumwombea baraka.

Viongozi hao walikutana mkoani Dar es Salaam, kwa ajili ya tukio hilo na Rais Samia alipiga simu ili kuwashukuru kwa jambo hilo jema kwenye maisha yake.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walitoa ujumbe kwa Rais Samia kumtaka kuendelea kufanya kazi kwa bidii, huku wakiahidi kuendelea kumwombea na kuliombea taifa ili liendelee kudumu katika upendo, umoja na mshikamano.

Mgeni rasmi katika tukio hilo, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, mbali na kumwombea dua Rais Samia, alimtaka kuendelea kutekeleza aliyopanga na wasaidizi wake badala ya kusikiliza lawama za watu.

Pia aliwataka Watanzania kukubaliana na mapenzi ya Mungu aliyopanga kwamba Rais Samia aongoze taifa la Tanzania na kuacha lawama kwa sababu yaliyotokea ni mipango ya Mungu.

Naye Kiongozi wa Kanisa la Tutashinda, Antony Lusekelo, aliwataka vingozi wa dini nchini kuhubiri amani na kuepuka kutoa mahubiri ya kukashfu au kuumiza dini nyingine.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kuwa sehemu ya kujenga umoja na mshikamano wa nchi, hivyo kwa kutumia lugha za kuudhi dini nyingine kutachangia mtengamano kwa taifa.

Aidha aliwahimiza viongozi wa dini kuendelea kuwaombea viongozi wastaafu kwa sababu walifanya kazi kubwa ya kujenga nchi na busara zao zinahitajika kwa ustawi wa nchi.

Lusekelo alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na viongozi wazuri ambao walifanya kazi kubwa ya kuliongoza taifa na bado wameendelea kuwa msaada mkubwa, tofauti na mataifa mengine ambako hawana umoja huo.

Naye Rais Samia, alipata fursa ya kuwasilisha shukurani zake kwa tukio hilo kwa njia ya simu, wakati akifuatilia kwa njia ya Luninga.

Rais Samia alisema: "Nawaona, naomba nisalimie hadhara iliyopo, nimewiwa kupiga simu nilivyoona kwenye TV ili niwashukuru sana kwa jambo mlilofikiria kulifanya viongozi wa dini. Nimefuatilia na nimesikia yale yote mliyoniombea nami namuomba Mungu asikie dua zenu ili niweze kulitumikia Taifa hili kwa sasa na badaye".

Aidha, Rais Samia aliwaahidi viongozi hao kuwa yupo pamoja nao katika kuliongoza Taifa na anaamini kuwa dua zao ndiyo zitamfikisha alipopanga afike.

"Naomba mwendelee kuwa name, naomba mwendelee kuniombea na ninawashukuru sana kwa hili kubwa mlilolifanya kwangu, asanteni sana," alisema Rais Samia.



Sehemu ya vijana 80 wanaotoka kwenye familia zinazoishi katika mazingira magumu ambao ni wanufaika wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), wakiwa katika majadiliano ya vikundi, wakati wa mafunzo ya ujasiliamali wa ufugaji wa nguruwe, katika kituo cha yatima Igoda, Wilayani Mufindi, mkoani Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Utafiti kubaini ufaulu duni Hisabati

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adoph Mkenda, amesema Serikali iko katika utafiti kubaini sababu za ufaulu usioridhisha katika baadhi ya masomo hasa Hisabati, ambalo limekuwa janga kubwa.

Aliyasema hayo jana wakati wa utoaji wa motisha kwa walimu waliochangia kiwango cha ufaulu katika somo la Hisabati jimbo la Ubungo na kwa wanafunzi waliopata daraja A na B.

Programu maalumu ijulikanayo kama KiuHisabati (Kuchochea Kiu ya kujifunzia Hisabati) ilianzishwa mwaka jana na Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, ambayo ililenga mwalimu ambaye mwanafunzi wake atapata A katika somo hilo aliahidiwa kupewa Sh. 100,000.

Kupitia programu hiyo, mwanafunzi aliyepata alama A na B katika somo hilo ameahidiwa kulipiwa ada katika masomo ya kidato cha tano na sita kama atajiunga na shule ya sekondari ya serikali .

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Mkenda alisema tatizo katika somo la Hisabati nchini ni kubwa, hivyo wanafanya utafiti ili kujua pia ubora wa kile alichopata mwanafunzi husika. "Kwenye Hisabati hali si nzuri, haturidhiki nayo kabisa, ufaulu ni mdogo, vigezo tunavyotumia vinaonyesha Hisabati tunafanya vibaya, ukiangalia mwaka jana ufaulu ulikuwa wa asilimia 20 lakini mwaka huu umekwenda asilimia 18.54. hili ni janga lazima tuchukue hatua za haraka,' alisema.

Prof. Mkenda alisema nchi zilizoendelea wanashindana uwezo wa kufaulu hasa kwenye Hisabati na kutolea mfano Japan na Marekani ambazo hufanya hivyo.

Alimpongeza Prof. Mkumbo kwa ubunifu huo wa kutoa motisha kwa walimu wa Hisabati na wanafunzi ambao sasa wanalipiwa ada.

"Dk. Sylvester Rugeihyamu (Mkuu wa Idara ya Hisabati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam- UDSM), hiyo fedha uliyosema ya kufanya utafiti katika somo la Hisabati kama haitoshi mje wizarani. Fanyeni utafiti na mtupe picha halisi ya nchi nzima, tufanye nini ili tuwezeshe wanafunzi waelewe zaidi. Tunawawezesha vipi walimu, nini kikwazo.

"Nitatoa fedha za wizara ili mripoti kwangu, tayari nimeshawahimiza baadhi ya wataalamu wafanye kwa ujumla wake, matokeo yote tumeyaona, kuangalia tofauti ya ufaulu inatokana na nini,' alisema.

"Ziko taarifa tunakusanya kila mwaka, tunataka kujua aina ya madarasa yaliyopo, walimu waliopo na wamepataje mafunzo. Tutatumia matokeo ya mwaka huu. Pia nitakaa na wamiliki wa shule binafsi tunajua ufaulu wao ni mzuri," aliongeza.

Kadhalika alitumia fursa hiyo kuhimiza walimu waandike vitabu vya kufundishia na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuangalia mitaala iliyopo.

Prof. Mkumbo alisema baada ya kuanzishwa kwa programu hiyo idadi ya ufaulu wa alama A wa somo la Hisabati jimboni humo umeongezeka kutoka sifuri mwaka 2020 hadi kufikia 30 mwaka 2021 na daraja B kutoka tisa mwaka 2020 hadi 31 mwaka 2021.

"Kiwango cha ufaulu katika somo hili kilikuwa cha juu kidogo asilimia 2.58 kwa shule zilizokuwa katika programu ya motisha kwa walimu ukilinganisha na shule ambazo hazikuwekwa kwenye programu hii ambazo ni asilimia 1.20," alisema.

Alisema walimu 30 wamepatiwa tuzo ya jumla ya Sh. milioni tatu na katika fedha hizo kila mwalimu aliyewezesha ufaulu amepewa Sh. 100,000.

Kwa wanafunzi waliopata daraja B katika somo hilo, alisema watalipiwa nusu ada katika masomo yao ya kidato cha tano na sita na waliopata daraja A, B na C pamoja na walimu wao watapelekwa mbuga ya wanyama ya Saadani Juni na Julai, mwaka huu.

## Serikali kutatua changamoto TMA

**Na Faustine Feliciane**

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imesema itaanza kuzifanyia kazi changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) likiwamo suala la mishahara.

Akizungumza wakati wa majumuisho ya ziara yake kwenye ofisi za TMA, Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema amezichukua changamoto zote zilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi.

Awali, akizungumza kabla ya naibu waziri huyo, Dk. Kijazi alisema pamoja na utendaji kazi mzuri wa mamlaka hiyo, ziko changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wafanyakazi. "Baadhi ya changamoto tunazokabiliana nazo ni upungufu wa vifaa vya kisasa pamoja na maslahi duni kwa wafanyakazi," alisema.

Dk. Kijazi alisema pamoja na changamoto hizo bado wameendelea kuwapatia uwezo wafanyakazi wao pamoja na kuboresha miundombinu ya hali ya hewa.

Naibu Waziri Mwakibete alisema kuelekea kwenye maandalizi ya bajeti mpya ya serikali, amezichukua changamoto hizo zilizoainishwa na ataziwasilisha sehemu husika.

Aidha, alitaka TMA kusomesha wafanyakazi kupitia miradi mbalimbali ya kimaendeleo ambayo inashiriki ili kuwa na wataalamu wabobezi wengi zaidi. Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mwakibete alitoa maelekezo kwa TMA ya kuwataka wafanyakazi kufanya kazi kwa kushirikiana.

"Haya ninayoyasema nimeona mnayafanya lakini nataka niwasisitize muyaendeleze zaidi, lakini pia suala la kutunza siri za ofisi ni muhimu, isitokee kila mnachokijadili kwenye vikao vyenu akatokea mtu mmoja akavisema nje ya utaratibu," alisema Mwakibete.

Pia aliipongeza TMA kwa kutoa utabiri sahihi ambao unaleta tija kwa Taifa na kuwataka kuendelea kusaidia jamii kwenye taarifa na kuwaepusha na majanga mbalimbali.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Dk. Burhan Nyenzi, alisema wamekuwa wakiisimamia vyema TMA ili huduma zake zikidhi vigezo vya kimataifa.

HABARI KITAIFA

# Wahujumu miundombinu ya serikali waonywa

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Wafanyabiashara wa Chuma Chakavu nchini (TSDA), imelaani kitendo kinachofanywa na baadhi ya watu wanaohujumu miundombinu ya serikali kwa kivuli cha biashara ya vyuma chakavu.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mwanasheria wa TSDA, Robert Sabini, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu vitendo vya uhujumu wa miundombinu ya serikali vilivyokithiri nchini.

Alisema iwapo itawabaini watu hao, itawachukulia hatua kali ikiwamo kuwafungulia mashtaka.

Sabini alisema wakiwa kama jumuiya ya wafanyabiashara ambao wanajihusisha na vyuma chakavu, hawawezi kulifumbia macho suala hilo.

"Tumeamua kufanya hivyo kwa kuzingatia kwamba, biashara hii ndiyo msingi wa kipato chetu, kuendesha maisha yetu na kusomesha watoto wetu.

"Kunapotokea kundi la wahalifu na kujiingiza katika tasnia hii, kwa kigezo kuwa ni wafanyabiashara wa chuma chakavu, wakati siyo wafanyabiashara au huenda ni wafanyabiashara lakini hawafuati kanuni na taratibu za nchi.

"Kwa hiyo, sisi tunawaonya wale wote wanaojihusisha na vitendo vya kuhujumu miundombinu ya serikali kwa kigezo cha biashara ya vyuma chakavu, tutawashughulikia na wala hatutakaa kimya," alisema.

Sabini ambaye pia ni Katibu wa TSDA Mkoa wa Tanga, alisema iwapo watawabaini wafanyabiashara hao, watawakamata kwa kutumia vyombo vya usalama na kuwafikisha mahakamani.

Aliongeza kuwa hawatasita kuisaidia serikali iwapo itatokea suala lolote la miundombinu kuhujumiwa.

"Kama serikali imetuamini na kutupa kibali cha kufanya biashara hii, sisi kama jumuiya tutaisaidia serikali kupambana na wahujumu hao,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa TSDA, Victor Masanja, alisema chuma chakavu ni masalia yenye asili ya chuma ambayo yanaweza kuendelezwa kwa matumizi mengine.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa jumuiya hiyo ni kwa ajili ya kuifanya biashara hiyo iweze kutambulika kwa jamii na kufanyika kwa kufuata taratibu na kanuni za nchi.

Alisema: "Kwa sababu biashara hii ilikuwa inafanyika kiholela, tumeona ni wakati muafaka sasa ifanyike katika misingi inayokubalika na jamii, wananchi na kushirikiana na serikali."



Mtaalamu wa mambo ya Tehama, Dk. Dennis Mwigusa akitoa mada kwa njia ya mtandao jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu idadi ya wafanyabiashara wanaotumia mtandao katika kazi zao nchini, baada ya utafiti uliofanywa na taasisi ya Stipro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utafiti wabaini wanawake wanatumia intaneti kidogo

**Na Gwamaka Alipipi**

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STIPRO), umeonyesha kwamba wafanyabiashara wanawake wanatumia kidogo huduma ya mtandao katika biashara zao kulinganisha na wanaume.

Akizungumza na waandishi wa habari, kiongozi wa utafiti huo kutoka STIPRO, Dk. Dennis Mwigusa, alisema utafiti huo ulifanyika mwaka jana na kuonyesha kwamba asilimia 48.8 ya wafanyabiashara wanawake huduma ya mtandao siyo lazima kwao na kwamba baadhi yao walieleza huwaongezea gharama katika shughuli zao.

Dk. Mwigusa alisema dhumuni la utafiti huo ilikuwa ni kukusanya taarifa kutoka kwa wamiliki wa biashara, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kufahamu changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao mtandaoni.

Alisema: "Tuliwahoji wafanyabiashara 63, kati ya hao 30 walikuwa ni wanaume na 33 walikuwa ni wanawake. Ilitumika njia ya kuwauliza maswali na kuchukua taarifa zao," alisema Dk. Mwigusa.

Alisema matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa wafanyabiashara waliokuwa na elimu ya shahada walikuwa ni asilimia 41.3, huku asilimia 30.2 walikuwa na elimu ya stashahada, asilimia 14.3 walikuwa na elimu ya cheti na asilimia 44.9 walikuwa na elimu ya sekondari.

Alisema pia matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa asilimia 27 ya wafanyabiashara walikuwa wanapata kipato cha Dola za Marekani 44 kwa mwezi, huku asilimia 25.4 kipato chao kilikuwa ni Dola za marekani 44 hadi 217 na asilimia 23.8 walikuwa na kipato cha Dola za Marekani 217 hadi 434 kwa mwezi.

# Waziri ahimiza elimu utunzaji mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema bado kuna umuhimu mkubwa wa kutoa elimu kwa Watanzania walio wengi kufahamu umuhimu wa kutunza mazingira ili yawe endelevu kwa vizazi vijavyo.

Hayo yalisemwa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamis Hamza Chilo, alipotembelea Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC).

Naibu Waziri huyo alifanya ziara hiyo kwa lengo la kujua majukumu ya baraza hilo na changamoto zilizopo kwa ajili ya kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema bado wananchi wengi hawajafahamu umuhimu wa utunzaji wa mazingira, hivyo taasisi zinazohusika kama NEMC zina wajibu mkubwa wa kuhakikisha zinawafikia wananchi na kuwapa elimu hiyo.

Mbali na kujifunza kazi za baraza hilo, Chilo alisema amebaini changamoto nyingi zinazosababisha uharibifu wa mazingira ambazo viongozi wa ngazi za juu wanapaswa kuingilia na kuchukua hatua stahili.

Naibu Waziri alisema bado kuna changamoto ya kimazingira kwenye uchimbaji madini, masoko, kwenye mikusanyiko ya watu, viwandani, vyombo vya usafiri na kwenye misitu ambako alisema watu hawana elimu ya mazingira na bado wanaharibu mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema ujio wa naibu waziri kwenye baraza hilo ni faraja kwani wamekuwa wakipokea miongozo na taratibu kutoka kwao.

"Kwa mara ya kwanza tumepata Naibu Katibu Mkuu wa wizara hivyo tunaamini mambo mengi yatakwenda kwa kasi na yatapata ufumbuzi kwa muda mfupi sana na kasi ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira itaongezeka," alisema Dk. Gwamaka

Alisema bado kuna changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira kama kelele na uchafuzi wa mito na aliomba wananchi kutoa taarifa kila wanapoona uharibifu wowote wa mazingira.

"Nchi ni kubwa NEMC haiwezi kuwa kila mahali wananchi mnaokaa sehemu zenye kero shirikianeni na baraza ndipo itakuwa rahisi kuzipatia ufumbuzi na hivi sasa tumepata nguvu mpya ya Naibu Waziri na Naibu Katibu Mkuu mambo yataenda kwa kasi," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Mwinyi kuhusu bima ifanywe kisheria

**WIKI** hii Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alifungua mkutano wa bima kwa nchi za Afrika, uliofanyika katika Hoteli ya Madinat Bahr, Mbweni jijini Zanzibar huku akizitaka kampuni zinazojihusisha na sekta hiyo kuwekeza Zanzibar ili kuwahudumia wawekezaji wanaomiminika kutokana na fursa zilizotangazwa na serikali.

Dk. Mwinyi katika hotuba yake hiyo alisema serikali haitopenda wawekezaji wanaowekeza katika sekta za utalii, bandari za kisasa, uvuvi, mafuta na gesi, wanakata bima kupitia kampuni za nje.

Bila kuuma maneno, Rais Mwinyi alisema serikali itahakikisha wawekezaji hao wanakata bima zao Zanzibar kwa ajili ya kinga juu ya uwekezaji huo na kwamba kwa kufanya hivyo, itachangia kukua kwa uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Kiongozi huyo alisema lengo la kufanya hivyo ni kujenga na kuendeleza uchumi wa kisasa na pia kutoa fursa ya uwapo wa mfumo, sheria na taratibu madhubuti za uendeshaji wa shughuli za bima, hivyo kuwapa wawekezaji imani na uhakika wa usalama wa mitaji wanayotaka kuwekeza.

Kauli hiyo ya Rais Mwinyi imetolewa wakati mwafaka ambao Zanzibar iko katika mkakati wa kuendeleza sera ya uchumi wa bluu kwa kutumia rasilimali zilizopo visiwani humo hususan katika sekta za gesi na mafuta, uvuvi wa bahari kuu, matumizi ya rasilimali za bahari na sekta ya utalii.

Ili kuhakikisha azma hiyo inatimia, serikali ya Zanzibar chini ya Dk. Mwinyi, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuvutia wawekezaji ili kuendeleza sekta ambazo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa visiwa hivyo. Hivi karibuni kwa mfano, serikali ilikodisha baadhi ya visiwa vidogo kwa wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza sekta ya utalii na mambo mengine ya kiuchumi.

Kwa mantiki hiyo, wawekezaji hao wanatumia fedha nyingi katika kuweka vitega uchumi vyao, hivyo suala la bima ni la muhimu katika kujilinda na majanga yanayoweza kutokea wakati wowote.


Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba hivi karibuni kumekuwa na majanga ya moto visiwani humo ambayo pamoja na mambo mengine, yamesababisha madhara makubwa kwa baadhi ya hoteli za kitalii.

Wawekezaji kukata bima Zanzibar ni jambo la kuungwa mkono kwa sababu kwa kufanya hivyo kuna manufaa makubwa ikiwamo kuchangia ukuaji wa sekta ya bima na uchumi kwa ujumla. Fedha zinazotumika katika kukata bima zitabaki nchini badala ya nchi zingine, hivyo kuwezesha pia kupanua wigo wa ajira kwa vijana.

Rais Mwinyi ameliona hilo kutokana na athari ambazo zimekuwa zikipatikana kutokana na kuwapo kwa mianya mbalimbali hususan baadhi ya wawekezaji kuweka fedha katika benki za nchi wanazotoka pamoja na masuala ya bima. Hatua hiyo inazinufaisha nchi zao.

Kauli hiyo ya Dk. Mwinyi inapaswa kuungwa mkono na kutekelezwa kwa vitendo. Pamoja na hayo, ili azma hiyo itekelezwe, ni vyema ukawasilishwa muswada wa sheria kwa ajili ya kuzibana taasisi zinazowekeza kufanya hivyo badala ya suala hilo kukaa bila msingi wa kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuondoa maduka ya dawa karibu na hospitali za umma sawa, lakini..

Na Sabato Kasika

**WIZARA** ya Afya imetoa miezi mitano kwa maduka binafsi ya dawa yaliyo nje ya hospitali, vituo vya afya na zahanati za umma, kuwa umbali wa mita 500 kama kanuni ya mwaka 2020 ya uanzishaji wa maduka ya dawa inavyoelekeza.

Hatua hiyo inaelezwa na Waziri wa wizara hiyo, Ummy Mwalimu kuwa, uwepo wa maduka yanachangia udokozi wa dawa na yanaondoa imani kwa wananchi kwamba hakuna usimamizi mzuri wa dawa vituoni.

Waziri anasema, maduka hayo yapo kinyume cha kanuni ya famasia iliyowekwa mwaka 2020, na kwamba baada ya miezi hiyo mitano maduka hayo hayatakiwi kuwapo karibu na maeneo ya kutolea huduma za afya.

Katika maelezo yake, Waziri huyo anasema, anatuma salamu maduka yote ya dawa lazima yawe mita 500 kutoka ndani ya hospitali, na kwamba atayaondoa ifikapo Julai Mosi, mwaka huu.

Sababu kuu za kuchukua hatua hiyo, ni kwamba huenda maduka hayo ya dawa yanahusika katika kuchochea upungufu wa dawa na vifaa tiba kwenye hospitali za umma hivyo kujenga taswira mbaya kwenye jamii.

Hatua hiyo inayochukuliwa na wizara ni nzuri kwa ajili ya kudhibiti wizi wa dawa katika hospitali za umma, lakini pamoja na hayo, ninadhani hiyo si njia tu ambayo inaweza kusaidia kudhibiti vitendo hivyo.

Kama mtu anaiba dawa hizo na kupeleka katika duka la karibu na hospitali, kituo cha afya au zahanati, hata maduka hayo yakihamishwa na kupelekwa mbali, bado vitendo hivyo vinaweza kuendelea.

Njia ambayo ingesaidia kumaliza tatizo hilo, kuweka mitego mbalimbali ya kudhibiti vitendo vya wizi wa dawa katika hospitali za umma, kwani serikali ina mkoni mrefu, hivyo inaweza kufanikisha hilo.

Vilevile si vibaya ukaguzi wa hali ya juu ukafanyika kwa watumishi wakati wanapotoka kazini kabla ya kuvuka geti, ili kubaini kama wanahamisha dawa kupeleka katika maduka yao.

Kwenye suala la wizi, ninaamini kuwa, dawa zikishaibwa na kutolewa nje ya hospitali zinaweza kupelekwa popote hata nje ya mkoa husika, hivyo sidhani kwamba ni lazima zikauzwa katika maduka ya jirani na hospitali.

Hivyo, kuhamisha maduka hayo kwenda mbali, ni sawa, lakini kuna changamoto zake hata kwa wagonjwa, kwani wakati inawezakana hospitali kukawa hakuna dawa, hali itakayomlazimu akanunue nje ya hospitali.

Iwapo maduka yatakuwa mbali, maana yake ni kwamba, mgonjwa au ndugu zake wanakuwa na kazi ya ziada ya kwenda nusu kilomita kununua dawa ambazo zimeelekezwa na madaktari.

Ingekuwa vyema iwapo hospitali zote zitakuwa na dawa na vifaa tiba vyote muda wote kwa mwaka mzima, huku watumishi wote wa umma wasio waaminifu wakidhibitiwa wasipate upenyo wa kufanya udanganyifu.

Kama kuna mianya katika mfumo wa udhibiti wa dawa zinazoingia na zinazotoka ili kutumika, basi uimarishwe kuziba mianya hiyo inayosababisha watu waamini kuwa dawa hizo zinauzwa katika maduka ya jirani.

Ninaamini kwamba, kama wapo watumishi wasio waaminifu kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati za umma, umbali wa mita 500 hauwezi kuwa kikwazo kwa watu hao kuhamisha dawa za umma.

Kwanza kabisa, nieleweke kuwa sina duka la dawa, lakini ninaamini kuwa uwepo wa maduka ya dawa karibu na maeneo ya umma ya kutolea huduma za afya, unasaidia upatikanaji wa dawa kirahisi.

Ikumbukwe kuwa, wakati mwingine wagonjwa hununua dawa na vifaa tiba katika maduka binafsi, kutokana na kutokuwapo kwa vitu hivyo ndani ya hospitali au kukwepa foleni katika malipo na mahitaji ya dharura.

Hivyo, ingekuwa ni vyema iwapo mkazo ungewekwa katika kudhibiti watumishi wasio waaminifu ili kukomesha vitendo vya wizi wa dawa kwenye hospitali za umma badala ya kupeleka mbali maduka hayo.

Kimsingi, sidhani kama kuna mgonjwa anayependa kwenda katika maduka ya nje ya hospitali kutafuta dawa au vifaa tiba, ila wakati mwingine changamoto kwenye hospitali za umma ndizo zinazo sababisha hali hiyo.

## SAFU/MAKALA

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Pongezi Bunge kuondoa ubatili kuhusu kujiuzulu kwa Ndugai



Na Pascal Mayalla

SERIKALI haiwezi kukosea jambo lolote lakini kwa vile serikali inaongozwa na watu, hao wanaoongoza serikali ni binadamu na si malaika, hivyo wanaweza kukosea. Watu hao wanapokosea, inahesabiwa ni serikali ndiyo imekosea.

Pia serikali inapofanya makosa huwa kunatokea watu wanaoikosoa kwa kutumia ukosoaji wa ujengaji (constructive criticism) ambao hufanyika kwa kuonyesha kosa lililofanyika na wakati huo huo katika ukosoaji huo, huandamana na ushauri juu ya nini kifanyike ili kurekebisha makosa hayo na maisha yaendelee.

Naishauri serikali yetu tukufu, pale inapokosolewa kwa makosa ya wazi, kwanza isikasirike. Pili, ifuate ushauri na kurekebisha makosa. Kukubali kosa na kupokea ushauri si udhaifu bali ni uimara.

Katika moja ya makala zangu zilizotangulia nilishauri viongozi wa kisiasa na wa serikali wanapofanya makosa ya wazi na kuifanya serikali ionekane imekosea, wanapaswa kwanza kukubali makosa, kuomba msamaha na kuwajibika. Hiki ndicho kilichofanyika kwa Spika aliyejiuzulu, Job Ndugai. Kwanza alikubali makosa, kisha akaomba msamaha na mwisho akawajibika.

Taarifa ya kujiuzulu Ndugai kwa vyombo vya habari iliyosambazwa na ofisi ya Bunge, ilionyesha ameandika na kuielekeza kwa Katibu Mkuu wa CCM na nakala ofisi ya Bunge. Msemaji wa Katibu Mkuu wa CCM alikiri kuipokea barua hiyo na Ofisi ya Bunge ikakiri kupokea nakala ya barua hiyo.

Barua hiyo ya kujiuzulu ilisababisha mjadala mkubwa wa kwa nini ipelekwe CCM badala ya ofisi ya Bunge kama katiba inavyoelekeza. Mjadala huo ulihitimishwa na taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa alichokifanya Ndugai kuandika barua CCM badala ya Bungeni ni sawa tu. Nami nikaweka ukosoaji wangu lakini ulikuwa 'constructive criticism' kwa kukosoa na kushauri kitu sahihi cha kufanyika.

Nilisema jambo fulani likielekezwa na katiba namna ya kufanyika, hakuna tena mjadala lifanyikaje. Ni lazima lifanyike kwa jinsi ile ile katiba ilivyoelekeza. Likifanyika kinyume linakuwa batili au batilifu. Hivyo nilionyesha kifungu cha katiba kinachoelekeza Spika akijiuzulu barua yake ya kujiuzulu inaandikwa kwa nani.

Ibara ya 149 1 (c) ya Katiba imeelekeza Spika akijiuzulu, ataandika barua kuliarifu Bunge. Kitu kikishaelekezwa na katiba namna ya kufanyika, kikifanyika kwa namna nyingine yoyote kinyume cha katiba ni batili. Kujiuzulu halali ni kuandika barua kwa mamlaka yako ya uteuzi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Spika, ameandika barua ya kujiuzulu kwa Katibu Mkuu wa CCM na nakala kwa kwa Katibu wa Bunge. Katiba imeelekeza barua ya kujiuzulu Spika, itatumwa kwa Bunge. Kitendo cha kuandika barua na kuituma CCM kabla ya Bungeni, kumeifanya kuwa batili. Bila huo ubatilifu kuondolewa, barua hiyo imekuwa batili!

Katibu Mkuu wa CCM alitoa taarifa ya kupokea barua ya kujiuzulu Spika na tayari ameliarifu Bunge kuhusu kujiuzulu huko na Bunge limeipokea taarifa hiyo, hivyo hivyo ubatili wake na kuikubali. Kama Bunge ndio mhimili wa kutunga sheria, lisipofuata katiba kwa kuukubali ubatili, nani atafuata katiba?

Haki ya CCM kupokea barua ya kujiuzulu, ni kama Ndugai angejiuzulu uanachama wa CCM, hivyo kupoteza ubunge wake na uspika. Hapo ndipo CCM ingeliarifu Bunge. Lakini yote kwa yote, Mahakama Kuu imeamua kwamba alijiuzulu kwa kufuata utaratibu kutokana na shauri lililofunguliwa na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Pamoja na hayo, je, tukiruhusu Bunge letu tukufu kukumbatia ubatili katika madogo, ubatili huu ukihamia katika makubwa, nani atakuwa na jeuri ya kulihoji Bunge? Kutokana na hali hiyo, nilitoa ushauri ufuatao; -

- Japo Ndugai ameishajiuzulu uspika, kwa kuheshimu katiba, lazima ubatili katika barua yake ya kujiuzulu uondolewe kwa kuandikwa barua rasmi kwa mujibu wa katiba.

- Kwa vile tayari CCM imeshakiri kuipokea barua, Bunge nalo limekiri kuipokea barua kutoka CCM, marekebisho ya kuondoa ubatili huu yafanyike kimya kimya. Spika mstaafu aelekezwe kuandika barua nyingine na Bunge lipokee kimya kimya barua mpya ya kujiuzulu iliyoandikwa kwa mujibu wa katiba, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na CCM ipewe nakala.

Serikali yetu ingekuwa inakubali makosa na kufuata ushauri, hii sintofahamu yote hadi kufikishana mahakamani, tusingefika huko kote. Hili jambo lilikuwa dogo tu. baada a Bunge kutoa taarifa ya kujiuzulu kwa Spika Ndugai ikionyesha ameandika barua CCM, badala ya Ofisi ya Bunge, Bunge lingetoa taarifa ya pili kuonyesha kulifanyika kosa kwa barua kuelekezwa CCM na kuonyesha kuwa barua imeandikwa kwa Katibu wa Bunge na nakala kupelekwa CCM.

Unapokosoa kwa kuandika na kushauri kitu cha kufanyika, halafu ukaona ushauri wako umefuatwa, makosa yamerekebishwa kama ulivyoshauri, huna budi kuandika tena na kutoa pongezi kwa serikali yetu kuwa sikivu na kuuondoa ubatili ule.

Kwa mantiki hiyo, nalipongeza Bunge letu tukufu kwa kuondoa ubatili wa barua ya kujiuzulu kwa Ndugai sasa imefuata katiba. Hongera sana kwa hili.

Sasa kumebakia ubatili mmoja tuu wa Naibu Spika, ajiuzulu kwanza unaibu Spika kabla ya kugombea Uspika na akiishajiuzulu unaibu spika, ndipo agombee Uspika.

**Wasalaam**
**Paskali**
**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tujiandae na kumbukizi ya Dk. John Pombe Magufuli



Na Joseph Kulangwa

**Kwa kasi hiyo, hivi sasa tunazungumzia kujengwa kwa bandari ya Bagamoyo, kwa kasi hiyo hivi sasa tunachanja chanjo ya Uviko-19 na kwa kasi hiyo hiyo, tunaona Lengai ole Sabaya akifungwa miaka 30 jela na akikabiliwa na msala mwingine.**

TUNA takriban mwezi na nusu hivi, tufanye kumbukizi ya kifo cha aliyekuwa Rais wetu kipenzi, Dk. John Pombe Joseph Magufuli aliyetutoka mwaka jana Machi 17.

Sijajua tutamkumbukaje 'classmate' wangu huyo, aliyetutoka huku tukiwa bado na mapenzi naye ya kusongesha gurudumu la maendeleo ya nchi hii tajiri, lakini yenye utajiri isiojua kuutumia!

Tangu aage Dunia, Dk. JPM, siku zinakimbia na Dunia inakwenda kasi ya ajabu. Nchi tunaambiwa imefunguka na mambo ni barabara kabisa na wapo wanaoonekana wameshamsahau.

Lakini tupo tunaomkumbuka bado kwa aliyotufanyia, tunashuhudia miundombinu ya barabara na madaraja alivyotuachia, tukijivunia. Pia viwanja vya ndege na madege yenyewe.

Nani asiyeona madaraja kama ya Patrick Mfugale pale Tazara, John Kijazi pale Ubungo, Tanzanite pale Aga Khan Hospital kuelekea Coco Beach na barabara za Patrick Mfugale pale Chamwino?

Nani asiyejua kuwapo kwa Mgufale Tower pale Chato, International Airport, Geita au Soko Kuu la Job Ndugai pale Dodoma, je, stendi kuu ya Magufuli pale Mbezi Luis, Dar es Salaam?

Hayo ni machache tu aliyotuachia mbali na bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere na reli ya kisasa vinavyoendelea kujengwa?

Mambo ni kasi na ni mwendo mdundo nakwambia.

Kwa kasi hiyo, hivi sasa tunazungumzia kujengwa kwa bandari ya Bagamoyo, kwa kasi hiyo hivi sasa tunachanja chanjo ya Uviko-19 na kwa kasi hiyo hiyo, tunaona Lengai ole Sabaya akifungwa miaka 30 jela na akikabiliwa na msala mwingine.

Nani alitarajia Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe atatinga mahakamani kukabiliwa na kesi ya ugaidi, nani?

Kwa kasi hiyo hiyo, tunasikia hivi sasa kuna mwingine akitafutwa kukabidhiwa samansi ili mwezi ujao naye tumwone kizimbani.

Hii kasi ni ya ajabu sana, nani alijua kuwa iko siku jamaa aliyemtishia bastola Nape Nnauye Machi 23, 2017 mbele ya Kanisa pale Oysterbay, atafikishwa kizimbani kwa tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara?

Hii kasi nakwambieni ni ya ajabu na ndiyo sababu watu huishia kusema tu kuwa acheni Mungu aitwe Mungu, kwa sababu kila kitu na mipango na wakati wake.

Mnakumbuka jamaa aliyemtishia Nape tulipohoji sisi vizabizabina kuwa ni nani huyo, tukajibiwa na mwanasiasa aliyekuwa na dhamana na Jeshi la Polisi, kwamba huyo si askari?

Leo Mungu akatuonesha kuwa kumbe jamaa ni polisi tena mwenye cheo aliyekuwa anasimamia mapolisi wenzake, baada ya kujisahaulisha kuwa lile la Nape limekwisha, kumbe Mungu alikuwa na jambo lake kwake.

Safari hii akaamua kumsogezea msala wa mfanyabiashara wa madini aliyeuawa Mtwara na kutoswa baharini, sijui kupoteza ushahidi, lakini Muumba ana yake, akamwibua na kumbe jamaa yetu ni mmoja wa watuhumiwa wa kumwaga damu ya mfanyabiashara huyo.

Jamani kila kitu kina muda na wakati wake, tunaona yaliyofanyika awamu ya tano mazuri na mabaya yake kama haya, yanakuja kuibuka katika awamu ya sita, ni ishara nzuri kwetu kuwa tunafunguliwa macho sasa.

Tunajifunza mengi, kuwa kumbe Dunia ni kubwa usifanye kitu au kumfanyia mwenzio ubaya, ukadhani maisha yatakuwa tambarare tu kila siku, hapana iko siku vilima na vibonde vitaibuka barabarani na utajikwaa tu.

Kuna siku utajisahau na kutembea peku na ndiyo siku utakutana na mbigiri barabarani zikuchome na ujute. Tunayashuhdia sasa,

watu wanakula mvua 30 jela, hatukujua kuwa walikuwa wakiyafanya haya huko nyuma, lakini Mungu saidia tumejua.

Lakini tumejua si kujua tu, lakini kujua kuwa kumbe waliyafanya wakikingiwa pengine vifua na wenye nguvu, lakini sasa Mungu akasema imetosha tufunue jungu tuone yaliyomo. Inshalah,

Allah ataendelea kutufungulia tuone mengi zaidi.

Tuanze tu maandalizi ya kumbukizi ya Dokta John Pombe Joseph Magufuli, ili hata kama ni kwa Ibada ya Kitaifa, basi na tuifanye katuachia mengi, mengi, mengi kama haya.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Manispaa ya Ubungo mjitafakari mgogoro huu hauleti afya kwenu



Na Thobias Mwanakatwe

INAFAHAMIKA kuwa urithi ni kitu chochote mtu anachokipokea kutoka kwa wazazi wake, wawe hai au wamekufa, hasa pale panapokuwa na uhusiano wa kindugu au kinasaba.

Ardhi ni moja ya mali ambazo zinaweza kurithishwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto au kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Sheria za mirathi, ziwe za kimila au serikali au zile za kidini, zinatambua suala la marehemu kurithisha ardhi yake kama sehemu ya mali zake endapo atafariki dunia.

Katika mazingira ya utekelezaji wa mirathi kuhusiana na ardhi, mali ile itagawanywa kwa mujibu wa maelekezo ya marehemu endapo atakuwa ameacha wosia au kwa maelekezo ya mila, dini au utaratibu mwingine kama hatakuwa ameacha wosia.

Sheria iko wazi kuwa baada ya kuthibitisha kifo cha marehemu ambaye alikuwa na umiliki wa ardhi au maeneo kadhaa, wanafamilia wanao wajibu wa kufungua shauri la mirathi katika mahakama yenye uwezo wa kusikiliza mashauri hayo. Mara nyingi mashauri hufunguliwa mahakama ya mwazo au mahakama kuu kulingana na ukubwa wa shauri na mali zinazohusika.

Baada ya ufunguzi wa shauri na kuorodheshwa mali za marehemu ikiwa ni pamoja na mashamba au ardhi, mahakama inao wajibu wa kumteua msimamizi wa mirathi endapo mhusika alifariki dunia pasipo wosia au mtekeleza wosia endapo aliacha wosia.

Nimeanza na utangulizi huo hasa kutokana na mgogoro wa ardhi kati ya familia ya marehemu Said Mziwanda ya Goba, Dar es Salaam na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Kwa jinsi nilivyofuatilia mgogoro huo, nimejiridhisha pasipo shaka kuwa hauna afya kwa Manispaa ya Ubungo kwa kuwa unaleta picha mbaya si tu kwa halmashauri bali pia kwa serikali. Kwa maneno mengine, unaleta uhasama baina ya jamii na serikali.

Hivi karibuni halmsahauri hiyo kupitia kwa Mkurugenzi wake ilisema haijawahi kupokea barua wala maelekezo kutoka kwa kiongozi wa juu serikalini kuhusu namna ya kutatua mgogoro wa ardhi kati ya manispaa na familia hiyo.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Beatrice Dominic, alitoa maelezo hayo baada ya familia ya marehemu Mziwanda kulalamika kuwa amepuuza kile walichodai maelekezo ya ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi iliyomtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa ashughulikie mgogoro baina ya familia ya Saidi Mziwanda na Roman Mosha. Katika ziara yake ya kutatua kero za wananchi aliyoifanya Agosti, mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitoa maelezo kuwa mgogoro wa ardhi unaohusu familia ya Mziwanda ulishatolewa uamuzi na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, William Lukuvi.

Akasema katika uamuzi wake, iliamliwa kuwa ardhi inayogombewa ni mali ya Manispaa ya Ubungo, hivyo kama familia ya Mziwanda inaona haijaridhika na uamuzi huo ni vyema ikaenda mahakamani na si vinginevyo.

Kauli hiyo ilipingwa na mmoja wa wanafamilia aliyemwomba Makalla kuonyesha vielelezo vinavyothibitisha umiliki wa manispaa na iwapo kulikuwa na maelekezo ya Waziri ya maandishi au ya mdomo juu ya uamuzi huo. Makalla katika majibu yake, alisema familia inatakiwa ifuate barua ya maelekezo hayo ndani ya wiki moja ofisini kwake.

Wakati mkuu huyo wa mkoa akieleza hayo, Chande alisimama na kueleza kuwa alipokea barua kutoka ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi ikielekeza kuwa mgogoro huo umeelekezwa ushughulikiwe na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. Makalla alijibu kwamba barua hiyo hajaipata na kama barua imeelekezwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara basi naye ataipata kwa utaratibu wake.

Mwanafamilia huyo katika mkutano wa hadhara wa Makalla alipokea barua ya 23 Agosti 23, 2021 yenye Kumb. Na. SAD.124/377/01/7 kutoka ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi iliyoelekeza kuwa mgogoro katika ardhi inayogombaniwa ni baina ya watu wawili, familia ya Mziwanda na Roman Mosha na kwamba katika barua hiyo manispaa haikutajwa.

Wakati mgogoro huo ukiwa bado haujapatiwa ufumbuzi, katika hali ya kushangaza, inadaiwa Manispaa ya Ubungo imeanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwa kuanza kuchimba eneo la shamba la familia licha ya kudaiwa kuna maelekezo ya barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi kuwa afike eneo hilo na kuutatua.

Mapema mwaka jana Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo alimshitaki msimamizi wa Mirathi, Salum Mziwanda katika Mahakama ya Mwanzo Kimara kwa madai kuwa wamevamia eneo la Manispaa. Mahakama ilipotaka vielelezo vya umiliki kutoka Manispaa, havikuletwa na hakimu aliyesikiliza shauri hilo alifuta kesi hiyo na kumwachia mshtakiwa.

Mgogoro huo uliwahi kufikishwa katika Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kinondoni na mmoja wa wanaogombania eneo hilo, Mosha aliyewashitaki ofisi ya Kata ya Goba, Manispaa ya Ubungo na familia ya Mziwanda kwa shauri Na. 318/2016.

Baadae Mwanasheria wa Manispaa ya Ubungo aliwasilisha maombi katika baraza hilo akiomba manispaa iondolewe katika kesi hiyo kwa kuwa haimiliki eneo hilo na hakuna kielelezo chochote cha umiliki na kwamba katika ufuatiliaji, walibaini ardhi hiyo ni mali ya Mosha.

Baada ya Manispaa kujitoa katika shauri hilo walibaki wawili, Mosha (mdai) na familia ya Mziwanda kama mdaiwa ambaye aliweke pingamizi la kisheria lililomshinda mdai. Baadaye tena Manispaa ya Ubungo iliibuka tena kudai eneo hilo ni mali yake na kuendelea kulishikilia hadi sasa na familia ya Mziwanda kumwandikia barua ya malalamiko Rais.

Mlolongo wa mgogoro huu ndio unatia shaka kwamba Manispaa ya Ubungo ambayo inapaswa kusimamia sheria ili mwenye haki apewe ardhi hiyo inaonekana kama ndiyo kichocheo.

Naiomba Manispaa isionekana chanzo cha kukwamisha mgogoro huu kupatiwa ufumbuzi kwa kuwa hali hii ikiruhusiwa kutawala itakuwa ni kuleta uchonganishi baina ya serikali na wananchi.

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# UMBEA, MAJUNGU VINAVYOWEZA KUSAMBARATISHA NDOA, FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KATIKA zama za sasa, tunaishi katika jamii ambayo ubinadamu unatawala hali ya ki-Mungu ndani ya binadamu. Watu wengi wamejeruhi wenzao kwa sababu ya kuendekeza umbea na majungu. Mambo haya yamewajeruhi, kuvuruga watu na kusababisha vifo katika jamii.

Umbea na majungu ni dhambi kama dhambi zingine. Umbea na majungu ni uovu, ubinafsi, aina ya ugaidi, upagani na ni dhambi dhambi kubwa kwa sababu huwajeruhi watu wengi, huharibu heshima na sifa za watu, huvunja uhusiano baina ya watu na marafiki na kusambaratisha familia na jamii. Umbea huzungumzwa kirahisi, husikilizwa kwa makini na kusambazwa kwa haraka. Mbaya zaidi, watu wengi huamini mambo ya umbea kuliko wanavyoweza kuamini mausia na mafundisho yenye kujenga.

Umbea na majungu msingi wake mkuu ni ulimi. Wakati mwingine ulimi umetumika kusema uongo na kuchafua mtu au watu kwa lengo la kuharibu. Mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari wakati mwingine vimetumika kusambaza habari za uongo na kuchafua watu. Mtu mmoja anapochafuliwa, hali hiyo haimhusu yeye tu bali familia, wazazi wake, ndugu na watu wengine wanaomtegemea.

Aidha, Umbea na majungu, wivu, husuda na chuki hujibainisha katika kutothamini kazi nzuri za wenzetu, kupinga sifa zitolewazo kwa mema waliyotenda ili kuhalalisha uzushi na kumdhalilisha mtu mwingine. Katika jamii tunayoishi wako watu ambao kazi yao ni kufitinisha watu wengine kwa kutafuta na kusafirisha habari.

Watu wa aina hii hupenda kusikia mambo ya wengine na kuyapeleka kwa wengine. Hali hii huvuruga amani na mshikamano katika familia na jamii. Umbeya na majungu ni dalili ya kufilisika kifikra na kimawazo. Umbeya na majungu ni hatari kwa amani na mshikamano katika familia na jamii kwani huchochea vurugu,fujo, mpasuko wa kifamilia na kijamii.

Kila mtu ajifunze kuwafikiria na kuwanenea watu wengine mema, kwani wema na ubaya ni akiba. Watu wasiendekeze umbea na majungu dhidi ya wale ambao hawawapendi au hawaelewani nao au wanaojisikia kuwa wanyonge kwao. Waheshimu watu wengine na usiwatendee wengine yale ambayo hupendi kutendewa. Apandaye mbegu ya fitina, atavuna zao la fitina yake.

Usiseme jambo kuhusu mtu mwingine, kwa kile ambacho huna ujasiri wa kusema mtu huyo akiwa mbele yako. Wanenee wengine yale upendayo wakusemee wewe. Unaposikia mambo ya umbea, usiyafurahie wala kuyachangamkia ili usishiriki dhambi hiyo.Mmbea na mpiga majungu anapoanza kusema mambo yake mkanye,muelimishe au badili mazungumzo au onesha kutokujali.

Jenga ukuta mkubwa masikioni mwako dhidi ya umbea, majungu na uzushi. Busara na hekima ya maisha inatudai kuzuia midomo yetu, kutawala ndimi zetu na kuepuka fitina. Umbea na majungu vimekuwa silaha ya watu waoga na dhaifu ambao hawathubutu kukabiliana na watu ambao wanahisi kutokuelewana nao au waliowazidi uwezo.

Umbea na majungu ni kichaka na maficho ya watu wavivu katika wajibu na kazi. Watu wa aina hii hawana muda wa kuchosha akili zao kufikiri na kubuni mambo yenye tija. Hivyo, dhamiri zao zinawasuta wanapoona wengine wakifanikiwa au kusifiwa kwa kazi njema.

Uhusiano mbaya baina ya dunia na wakaaji wake, baina ya Mungu na watu wake, baina ya ndugu na ndugu, waumini kwa waumini na watumishi kwa watumishi, ni matokeo ya tamaa ya vitu, hali, hadhi na heshima ambayo inaibua na kuchochea hali ya wivu, chuki na husuda inayojieleza na kujipambanua katika umbea na majungu. Umbea na majungu ni mtaji wa watu dhaifu na wasiojitambua.

Viongozi katika ngazi ya familia na jamii wanaalikwa kuwa sehemu ya suluhu na si tatizo. Viongozi tunapaswa kuwa sababu ya kuleta uponyaji katika dunia dhidi ya hali hii ya ugaidi wa umbea, majungu, uzushi na fitina. Viongozi wana wajibu wa kujenga uhusiano bora baina ya muumba na viumbe, baina ya watu na viumbe.

Viongozi kujiingiza katika umbea na majungu ni kujikosea na kuwakosea wanaowaongoza. Viongozi wanapaswa kuwa wapatanishi na watafuta maridhiano na suluhu juu ya changamoto. Mungu akusaidie kutoka kwenye uhaini wa umbea na majungu kwani si dili. Kumbatia upendo, utu wema na fadhili na utayari wa kutenda mema kwa binadamu mwingine ili Mungu akutakabali.

**●Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

JANUARI 30, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13


**Suruali hizi zitawafurahisha wanawake**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Maua yanavyochagiza mvuto wa nyumba



## HARUSI


Ukurasa 12




# Namna ya kuchonga pua yako

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | J | A | Z | W | A |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| A | M | A | ■ | K | ■ |
| ■ | B | ■ | D | A | U |
| ■ | I | ■ | ■ | T | ■ |
| T | A | M | B | I | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ONA, IBA, DIMBA, YANGA, BAMBIA, DONYOA

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Grace alikuwa shambani na mama yake akimsaidia kulima bustani ya mbogamboga, ghafla alimuona nyuki akiruka kutoka ua moja hadi lingine.

Grace alivyomuona yule nyuki alianza kumfuata kutoka sehemu moja hadi nyingine huku akirukaruka. Mama yake alipomuona alianza kumuuliza.

**Mama:** Mwanangu mbona unarukaruka?

**Grace:** Mama nimemuona nyuki najua nitakula asali

**Mama:** Kakuambia nani ukimuona nyuki utakula asali?

**Grace:** Mwalimu wetu alitufundisha kuwa Fuata nyuki ule asali, leo nitakula sana.

**Mama:** Hapana mwanangu, huo ni msemo tu unamaanisha kwamba kuwa karibu na watu ili unufaike baadhi ya vitu.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Je, umewahi kujihukumu mwenyewe?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada iliyopita kuhusu hatari ya kufa ndani yako. Nilieleza kuwa mwanadamu ni ndani na nje. Sasa kuna hatari ya mtu akafa ndani, kifo ambacho ni hatari zaidi.***

Ni hatari kwa sababu ndani ndipo unakaa moyo wa mtu. Ndani ndipo inakaa dhamiri (dhamira) ya mtu, utashi wa mtu. Dhamiri ya mtu inapokufa ni hatari sana!

Dhamiri maana yake ni kile kitu kilichoko ndani yako ambacho Mungu amekiweka kama kiashiria au niite alamu kama ya kwenye gari. Kitoa taarifa kwamba kuna kitu kimegusa gari au kukaribia eneo husika.

Sasa kiashiria kama hicho Mungu hukiweka ndani ya moyo wa mwanadamu. Hiyo alamu ndiyo tunaita dhamiri, kwamba ndani yako ukifanya kitu ukikosea, unasikia hukumu ndani yako! Dhamira inakusuta, inakushitaki kwamba hapa umefanya jambo baya, umekosea.

Msomaji wangu labda nikuulize; Umewahi kumpita mtu barabarani, hujamsalimia, kisha unageuka unarudi kumtaka samahani, na kujitetea kuwa ulikuwa kwenye mawazo hivyo hukumuona?

> **“Yupo mtu akisikia tu amesemwa ndipo utamjua mtu huyo amekufa au yu hai. Kama aliyemsema anakaa mbali, yuko radhi afunge safari amfuate ili amueleze vizuri kwa nini amemsema.**

Au pengine umemkosea mtu, umemjibu vibaya lakini baada ya muda ndani yako unajisikia kuhukumiwa. Ndani unajisikia vibaya kwamba kwa nini ulimjibu vile? Hiyo inatoka ndani yako.

Iko hatari mtu akawa amekufa ndani bila yeye kujijua. Mungu akasema hivi katika moja ya maandiko yake; “Bali yeye asiyejizuia nafasi yake, amekufa ingawa yu hai”. Maana yake ni kwamba upo uwezekano wa mtu akawa anatembea ingawa amekufa.

Kwa mantiki hiyo, kuna watu wamekufa ndani ingawa wanaongea kwa nje. Utawaona wanafanya kazi zao kama kawaida lakini wamekufa. Ndio maana nikasema kuwa kuna hatari ya kufa ndani pasipo kujua! Na mtu anayekufa, ni mtu ambaye siku moja alikuwa mzima. Hakuna kitu kinachoweza kufa wakati kilishakufa. Hakuna kufa mara mbili. Yaani unapomuona mnyama akiwa hai, siku moja anaweza kufa.

Tunapoongea kifo cha ndani maana yake tunaongea habari ya mtu ambaye ni mzima, yupo hai, anaona, anatembea na ndani yake yupo hai. Ndani yake anampenda Mungu, anamjua Mungu. Huyu ndiye aweza kufa.

Vile vile yawezekana ni mtu anayetenda maovu lakini alikuwaga hai, alikuwa mwombaji, mcha Mungu, ila leo ameacha. Mtu wa aina hii amekufa ingawa yu hai. Wapo watu ambao hawawezi kuzuia nafsi zao kwa jambo lolote lile. Kwa mfano hasira.

Roho ya hasira imesababisha majanga ya aina mbalimbali. Utaona watu wameketi kujadili jambo fulani, lakini ghafla mmoja ananyanyuka kwa hasira anatukana huku akitaka kupigana. Huyu ameshindwa kuzuia nafsi yake.

Yupo mtu akisikia tu amesemwa ndipo utamjua mtu huyo amekufa au yu hai. Kama aliyemsema anakaa mbali, yuko radhi afunge safari amfuate ili amueleze vizuri kwa nini amemsema.

Mara nyingi mwisho wa tafrani za aina hii huwa siyo mzuri. Watu huishia kuumizana au hata kuweka visasi vya muda mrefu. Yote hayo chanzo ni ghadhabu ya mtu mmoja aliyesemwa kuhusu jambo fulani, ambalo yawezekana ni kweli au kasingiziwa. Lakini mwisho wa siku likazua balaa kubwa!

Isitoshe, ipo misemo kwamba, pata pesa tujue jeuri yako au jenga nyumba au nunua gari tujue jeuri yako! Yupo mtu mnyenyekevu wakati hana kitu, ngoja apate ndipo utaona rangi zake zote. Ngoja apate kazi au apate katripu kwenda alaya arudi, utamjua vema. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Utajijua umekufa kwa kujichunguza nafsi yako. Ukimuona mtu ana maneno machafu, rudi ndani yake. Ndio maana tunaambiwa kuwa ‘kimuingiacho mtu siyo najisi bali kile kimtokacho ndiyo najisi!’

Mfano, mtu anajichimbia kaburi lake na kulisakafia vema na kuagiza akifa azikwe humo. Hilo ni wazo toka ndani yake sasa akaitoa nje dhamira yake, hivyo kuwaacha wengi midomo wazi.

Mtu wa aina hii ameshajiua ndani ya moyo, anasubiri kuzikwa rasmi kimwili ili kumbukumbu lake liwekwe kihistoria. Amejitafakari ndani akafanya hicho tunachokiona leo ni maajabu. Rudi ndani yako, kwa nini maamuzi ya aina hii yatokee? Lazima zipo sababu!

Bila shaka msomaji wangu umejifunza mengi. Niishie hapa kwa leo tundelee tena wiki ijayo. Je, una maoni? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Viongozi wa dini, kimila pazeni sauti mauaji haya

HAIPITI siku haijaripotiwa mauaji ya kikatili dhidi ya binadamu ambayo sababu nyingi ni wivu wa kimapenzi au dhuluma ambayo mtu anashindwa kuvumilia, hivyo anaona suluhisho ni kujiua au kumuua mwingine.

Matukio haya yameenda mbali kwamba sasa mtoto anamuua mzazi wake na kuuficha mwili wake na kote uchunguzi wa awali unaonyesha sababu ni kutaka kujipatia mali.

Mojawapo ya matukio hayo ni la jijini Arusha ambalo kijana wa kiume alimuua mama yake na kumtumbukiza kwenye shimo la choo. Likafuata tukio la binti kumuua mama yake akamzika mwaka mmoja uliopita. Kila akiulizwa anasema yuko nchini India kwa matibabu, huku yeye anauza mali taratibu.

Lingine ni la aliyekuwa Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kumuua baba yake kwa kile alichodai ameelezwa kuwa ndiye anayemloga. Matukio mengine ni mwanamume au mwanamke kumuua mpenzi wake kwa wivu wa mapenzi huku baadhi wakiacha ujumbe.

Tukio lililoshangaza wengi ni la mtu aliyekuwa anamdai mjamzito wa miezi minane Sh. 100,000 za mahindi kumuua kwa kumchinja, kisha kuwaua watoto wake wawili ambao walimwona wakati mama yao anachinjwa na wanamfahamu aliyetenda tukio hilo.

Yako matukio ya mtu kuua wanafamilia kwa sababu ya kudhulumiana na wengine hata hakuna sababu. Mathalani tukio la hivi karibuni Jijini Mwanza ambalo mama, mwanawe na binti wa kazi waliuawa na miili yao kutupwa mtoni. Aliyetekeleza mauaji alipokamatwa alisema ni kwa sababu ya kuona amedhulumiwa maharage aliyowauzia kwa mali kauli.

Haya ni baadhi ya matukio kati ya mengi yaliyotokea nchini kwa kipindi cha mwezi mmoja, ambayo mara nyingi mtu utajiuliza aliyetenda haya ni binadamu mwenye moyo wa nyama kama walivyo wengine au aliyemtendea tukio hilo?

Katika amri za Mungu, mojawapo inasema usiue lakini watu wanasahau kabisa na kuwaua wengine bila kujua kuwa damu ya mtu haipotei. Itakulilia kama ambavyo tunavyosoma kwenye vitabu vitakatifu jinsi damu za baadhi ya watu zilivyowalilia watu kizazi hadi kizazi.

Mfululizo wa matukio haya unashtua kwamba watu wanaona njia rahisi ni kumuua mwingine ambaye hawezi kuumba hata kiungo kimoja. Mbaya zaidi wauwaji hutambuliwa kwa haraka na hukamatwa kiasi kwamba kama alijipatia mali basi hatazifaidi na bado ana kesi ya kujibu mbele ya Mungu na vyombo vya sheria.

Kwa matukio haya, ni wakati sasa wa jamii kuamka kwamba kwenye maeneo yetu kuna viongozi wa dini, viongozi wa kimila na jamii wanapaswa kulibeba kama ajenda muhimu ya kuieleza jamii ubaya wa matukio hayo na namna yanavyoweza kuacha laana kwenye kizazi au eneo.

Ninatambua kuwa viongozi wa dini wana kamati ya amani ya kitaifa, hivyo naamini ina matawi hadi ngazi ya chini kabisa. Ni muhimu tuone sasa ikifanya kazi kwenye eneo hili kwa kuwa ni moja ya visababishi vya kupotea kwa amani.

Lazima viongozi hawa wenye ushawishi na wanasikilizwa na jamii wakapaza sauti zao kuzungumza mara kwa mara na wanajamii kupitia ibada na mikutano muhimu. Lakini ni wakati wa wanasaikolojia kupaza sauti na kutumia taaluma yao kuisaidia jamii kuondokana na ukatili huu ambao unailaani nchi.

Kila aliyepaza sauti kwa sasa amelitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua lakini tunasahau kuwa siku zote wanachukua hatua wanawakamata,wanapeleleza na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa, lakini bado hawawezi kufanya kazi wenyewe bali kwa kushirikiana na jamii.

Natambua wajibu mmojawapo wa polisi ni kulinda amani lakini tutambue kuwa wao ni wachache kuliko wananchi na wanapaswa kusaidiwa. Pamoja na kwamba watapewa taarifa watapeleleza, bado wanahitaji kusaidiwa na wanajamii wenyewe.

Nafasi ya viongozi wa dini, kimila na watu maarufu wenye kuheshimiwa kwenye jamii ni kubwa kwenye kuisaidia jamii iondokane na ukatili huu. Haitoshi polisi kulinda kwa kuwa hawawezi kulinda kila nyumba na hata wakifanya doria bado haiwezi kuzuia mtu kuingia ndani ya nyumba ya mwingine na kutekeleza mauaji.

Kwenye imani za dini tunafundishwa yako mapepo au mashetani ambayo humwingia mtu na kumsukuma kuumua mwingine. Haya hayadhibitiwi na polisi bali viongozi wa dini wenye imani thabiti wanaoweza kuyaombea yakatoka.

# HARUSI

Jambo la muhimu katika harusi za Kiafrika ni kumpamba uso bibi harusi ili apendeze zaidi. Pichani ni baadhi ya picha zinazoonyesha jinsi gani bibi harusi anavyoweza kupambwa na kumfanya awe na mwonekano tofauti.











# MITINDO

TWENDE NA JOTO

## Suruali hizi zitawafurahisha wanawake

MWELEKEO wa hali ya hewa unaonyesha tunaingia msimu wa joto katika kujiandaa mvua za masika miezi michache inayokuja.

Katika kipindi hiki joto linaongezeka kwa kasi na kusababisha mwili kuhitaji vitu vya ziada kuupooza wakati tukiwa katika shughuli zetu mbalimbali. Wataalamu wa mavazi, wanashauri kuwepo na uchaguzi mzuri wa mavazi hasa kwa wanawake ambao wanaathirika sana na joto.

Moja ya nguo ambazo wanatakiwa kuwa nazo ni suruali, wanashauriwa kuvaa za vitambaa na zenye uwazi mkubwa kwa ajili ya kusaidia mwili kupata hewa. Kwa sababu hii, suruali za mitindo, majira ya joto, inashauriwa kuvaa na blauzi za satini na blauzi nyepesi.


Kwa kuongezea, katika chaguzi za wanawake ni bora kuvaa suruali ya joto kuvaa na viatu vya wazi au raba na snika.







UREMBO







# Namna ya kuchonga pua yako

MAKE-UP inaweza kufanya mabadiliko makubwa kwa uso wako, ikiwa imefanywa vizuri.

Haishangazi kuona wataalamu wa kujipodoa na wasanii wa kutengeneza ambao wanaweza kufanya maajabu kwenye uso wako.

Sio lazima uchukue mkazo wowote kuhusu muonekano wako wakati unaweza kuunda muonekano wa 'kichawi' na kuficha kasoro zako zote za uso na uundaji mzuri uliofanywa.

Kuna vidokezo kadhaa vya kutengeneza ambavyo vitafanya pua yako ionekane ndogo na nyembamba. Vidokezo hivi ni rahisi kufuata nyumbani na hautahitaji mtaalamu yeyote wa kujifanya ili kufanya hivyo.

Kufanya pua yako ionekane ndogo ni suala tu la mbinu kadhaa za busara za kutengeneza.

Hata watu mashuhuri wengi hutumia mbinu za kujipiga 'make up' ili kuficha saizi ya pua zao kwa kutumia mapambo.

Hapa, tutashiriki nawe vidokezo rahisi lakini muhimu vya kufanya pua yako ionekane ndogo.

Ikiwa unataka pua yako ionekane nyembamba tumia msingi kwenye pembe za nje za pua yako.

Msingi lazima uwe na vivuli viwili vyeusi kuliko rangi yako ya ngozi ya asili. Baada ya haya, weka msingi mwepesi wa vivuli viwili kwenye daraja la pua yako.

### Tumia bronzer

Paka bronzer kwenye paji la uso wako, kidevu, mashavu, na chini ya katikati ya pua yako. Hii itafanya pua yako ionekane nyembamba na ndogo. Bronzer itaongeza asili kwa ngozi yako.

Epuka kutumia mapambo mazito ya macho

Ni kosa kubwa kufikiria kuwa utengenezaji wa macho wenye ujasiri utaunda umakini zaidi kwa macho yako.

Lakini kwa kweli kesi hiyo ni kinyume, utengenezaji wa macho mazito utazingatia zaidi pua yako.

Kwa hivyo ikiwa unataka pua yako ionekane nyepesi, basi nenda kwa mapambo ya macho ambayo yatatoa muonekano wa asili.

### Kufanya pua ndefu ionekane fupi

Unaweza kufanya pua yako kubwa ionekane ndogo kwa kutumia msingi. Paka rangi nyeusi ya msingi kwenye ncha ya pua yako na kati ya puani (chini ya pua yako).

Changanya msingi vizuri ili iweze kuonekana asili.
Tumia Mchanganyiko chini ya Macho

Miduara ya giza chini ya macho yako itaunda kivuli na hiyo itafanya pua yako ionekane kubwa zaidi.

Daima tumia kificho kufunika miduara ya giza na itafanya pua yako ionekane nyembamba.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jilambe kwa tambi za njegere na nazi

TAMBI zinaweza kupikwa kwa mapishi ya aina tofauti na kila pishi linakupa ladha tofauti.

Mapishi haya yanakuja na ladha tofauti kidogo kwa kuweka ladha ya nazi na njegere.

Njegere hukipa upekee chakula cha tambi na kuzifanya ziwe tamu zaidi.

Chakula kina harufu nzuri, muonekano mzuri na ladha tamu mdomoni.

Jaribu vitu tofauti kuongeza raha maishani kwako. Unaweza kula pamoja na kachumbari, nyama, samaki au kiambato chochote upendacho. Usisahau pia kuwa na kinywaji ukipendacho.

### MAHITAJI

Nazi moja, tambi, hiliki, sukari na njegere robo kilo.



### NAMNA YA KUANDAA

Tayarisha njegere kwa kuziosha na kuzichemsha hadi ziive.

Kuna nazi, kamua tui zito, menya hiliki kisha zitwange kwenye kinu.

Bandika maji jikoni na yakichemka tumbukiza tambi, toa kwenye maji dakika moja pungufu ya muda ulioshauriwa.

Hii inasaidia kufanya tambi ziwe ngumu ili kuweza kuiva vizuri ukipika na tui.

Weka tambi kwenye chujio ili zitoe maji.

Bandika tui jikoni weka hiliki. Koroga mchanganyiko ili kupata tui laini na kuzuia lisikatike.

Weka njegere kwenye tui na koroga ili ziweze kuchanganyika.

Ni vizuri kama utaponda njegere ili kupata rojo tamu kwenye mchanganyiko.

Tui likishachemka weka tambi na sukari huku ukiendelea kukoroga taratibu hadi tui likauke na kubaki mafuta.

Chakula kipo tayari kuliwa wakati wowote utakaojisikia kula iwe asubuhi, mchana au usiku.

MAISHA NI NYU

Na Elizabeth Zaya



# Maua yanavyochagiza mvuto wa nyumba

MVUTO na uzuri wa nyumba huchagizwa na vitu mbalimbali ambavyo hutegemeana na umaridadi au ubunifu wa mwenye nyumba mwenyewe au wanaoishi katika nyumba husika.

Vitu hivyo vinaweza kuwa vimebuniwa moja kwa moja wakati wa usanifu wa nyumba au baada ya ujenzi kumalizika na kuanza kutumika.

Leo tunaangazia namna maua yanavyochagiza mvuto au uzuri wa nyumba, iwe ni kwa ndani ya nyumba husika au nje bila kuchagua aina ya maua yenyewe.

Nyumba au nyumbani ndiko mahali ambako mtu hutuliza akili yake na kuanza kupanga namna ya kuendesha maisha yake, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kupafanya pawe mahala pa kuvutia na pa kutuliza akili na nafsi kwa ajili ya kuruhusu akili kutafakari sawasawa.

Ndiyo maana leo tukaangazia jambo mojawapo la umuhimu kwenye nyumba ambalo ni maua katika lengo lile lile la kupaweka nyumbani pawe pa mvuto na pa kuituliza akili.

Maua haya kwenye nyumba hususani kwa nje, yanaweza kutengenezwa au kupambwa kwa njia tofauti ama kwa mtindo wa bustani au yakawekwa moja moja kulingana na uchaguzi wa wahusika katika nyumba na kwa vyovyote vile yanavyowekwa huleta utofauti wa mvuto katika nyumba tofauti na ile ambayo haina maua kabisa.

Lakini kutengeneza maua katika mtindo wa bustani huleta mvuto zaidi na pia humvutia mtu au watu wanaoishi katika nyumba husika kupendelea kutumia eneo hilo kwa mapumziko na kuhuisha akili baada ya shughuli nyingi za kutwa katika kujitafutia ridhiki.

Lakini kama hiyo haitoshi, maua hutumika kama urembo ndani ya nyumba na yanaweza kurembwa kulingana na rangi zilizomo kwenye nyumba husika. Katika hili ni muhimu kuyaweka katika maeneo mahususi na si kuyaweka ilimradi yanapopangiliwa kwa ustadi huongeza mvuto zaidi.

Tukumbuke pia kwamba mbali na kuleta mvuto katika nyumba, pia maua yanatupatia hewa safi na harufu nzuri. Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa wa kuyatumia katika nyumba zetu.

Tusisahau kwamba tunapoamua kuyatengeneza maua kwenye nyumba zetu, tunahitaji kuzingatia kuyahudumia kila siku ili yastawi vizuri na si kugeuka kuwa karaha, uchafu au vichaka nyumbani.





## Namna ya kupangilia chumba chako kimoja na kikawa na mvuto



HAKUNA ubaya wa kuishi kwenye chumba kimoja kama uko mwenyewe na ndio unaanza maisha ya kujitegemea.


Kitu kitakachofanya chumba kimoja kukosa mpangilio ni mrundikano. Mrundikano unafanya mahali paonekane pachafu, ondoa mrundikano kwenye chumba chako ambapo kitaonekana kuwa na nafasi na kisafi.

Nunua au tengeneza kitanda, meza na sofa vyenye maeneo ya kuhifadhia kwa chini. Vitu hivi vinawezesha kuweka mpangilio pale vinapokuwa na maeneo ya kuhifadhia, yaani kitanda au sofa ambalo mvunguni kuna droo za kuhifadhia.

Kwenye chumba chako hicho kimoja weka kabati la nguo ambalo lina milango. Kwa ndani kwenye milango pigilia kulabu ambazo utatumia kutundika mikoba, mabegi na hata shanga na mikufu yako.

Ukiwa unaishi kwenye chumba kimoja uwe na vitu unavyohitaji kwa wakati husika tu. Huna haja ya kuwa na nguo, viatu na vyombo ambavyo huvitumii kwa wakati huo. Mrundikano wa vitu unavyotumia na usivyotumia utakuvuruga kiasi kwamba unashindwa kuona hata kile unachohitaji kutumia.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MWALIMU ANA-LALAMIKA HUNIFU-NDISHI 'KINGLEDHA' NIKITOKA SHULE
MWAMBIE... MUDA ANAORUDI BABA TOKA BAR NA KINGELEZA CHAKE ANANIKUTA NIMELALA
SIASA NI KAMA KUMCHINJA KOBE NIPO KIMYAAAA! NASUBIRI 'KIKI' NISHOBOKE
UNAJI-ENDESHA KWA SHOBO AU SIO?
DOKTA... MGONJWA WANGU 'ANA-ENDESHA BILA KUPUMZIKA!
OHOO! NI TRAFIKI KESS!
'NSHAJI-ZOELEA'
UTA-SEMAJE'
'SIMPO' NIKIFA NDUGU ZANGU WATAITWA 'NDUGU WA MAREHEMU' WATALIBEBA
'MIDENI'
RUDI KWA MKEO UKAMUOMBE RADHI KULALA NJE!
KIKWETU HIVYO MWIKO! ILA ANIULIZE AONE...
DALALI HUKU UNAKONIPELEKA 'INA CHOO CHA KUKAA?'
HADI CHA WIMA KIPO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
CHAWA WA ZAMANI SIO WA SASA...

HABARI KIMATAIFA

# Marekani kuongeza wanajeshi Ulaya Mashariki kuikabili Urusi

**WASHINGTON D.C** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema utawala wake umepanga kutuma wanajeshi zaidi huko mashariki mwa Ulaya, wakati nchi wanachama wa jumuiya ya kujihami NATO wakijaribu kuimarisha uwapo wakati wakikabiliana na tishio la Urusi.


Biden alitoa kauli hiyo juzi, akisema kwamba atapeleka wanajeshi hao katika eneo hilo siku chache zijazo, akiongeza kuwa idadi yao haitakuwa kubwa.

Jumatatu kiongozi huyo aliamuru wanajeshi 8,500 kuwa katika hali ya utayari ili waweze kusambazwa endapo watahitajika.

Alisisitiza kwamba hatua hiyo ni ya tahadhari katika kushughulikia changamoto za wanachama wa NATO wa Ulaya Mashariki.

Hata hivyo Marekani haitopeleka wanajeshi wake ndani ya Ukraine.

Kwa kawaida Marekani ina maelfu ya wanajeshi wake barani Ulaya ikiwemo askari 35,000 nchini Ujerumani.



Baadhi ya wanawake katika jimbo la Tigray nchini Ethiopia, wakisubiri msaada wa chakula kutoka mashirika ya kimataifa hivi karibuni. Asilimia 40 ya wananchi katika eneo hilo wanakabiliwa na ukosefu wa chakula **(PICHA: BBC)**

# Kiongozi AfD atangaza kujitoa

**BERLIN,** UJERUMANI

KIONGOZI mwandamizi wa chama cha siasa kali za mrengo wa kulia nchini Ujerumani cha AfD, Jorg Meuthen, ametangaza kujiondoa kutoka chama hicho ambacho alisema kinazidi kuchukua mwelekeo wa itikadi kali.

Meuthen ambaye alichaguliwa kuwa kiongozi mwenza wa chama cha AfD mwaka 2015, alisema sehemu kubwa ya chama hicho na wawakilishi wake wameamua kufuata mkondo wa msimamo mkali kisiasa.

Kwa muda mrefu mwanasiasa huyo amekuwa kwenye mivutano na wenzake ndani ya AfD, na katika kipindi cha miaka miwili iliyopita amekuwa akipigia upatu chama hicho kuchukua mwelekeo wa siasa za wastani.

Msimamo huo ulimtengenezea maadui na kupunguza ushawishi wake ndani ya chama hicho kilichopata umaarufu wake kupitia sera za kupinga wahamiaji.

# ECOWAS yasimamisha uanachama wa Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

JUMUIYA ya kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi, (ECOWAS) imetangaza kusimamisha uanachama wa Burkina Faso, katika jumuiya hiyo baada ya mapinduzi ya kijeshi.

Katika taarifa yake ilisema haitatangaza vikwazo vingine dhidi ya Burkina Faso ili kusubiri matokeo ya mazungumzo baina yake na viongozi wa kijeshi.

Wakuu wa jumuiya hiyo wamekubaliana kutuma ujumbe wake uliowasili jana mjini Ouagadougou, kabla ya viongozi kukutana tena Februari 3, nchini Ghana ili kutathmini matokeo ya mazungumzo yao.

Katika mkutano wake wa kilele kwa njia ya video uliodumu kwa saa tatu, viongozi hao pia walitoa wito wa kuachiliwa huru kwa Rais Roch Marc Kabore na viongozi wengine waliokamatwa.

Kiongozi wa wanajeshi waliotwaa mamlaka, Kanali Paul Henri Sandaogo Damiba, aliahidi kurejesha usalama na katiba nchini humo pale mazingira yatakaporuhusu.

# Mgombe urais Italia bado kitendawili

**ROME,** ITALIA

BUNGE la Italia limepiga kura jana kwa siku ya sita, kumchagua Rais, lakini bado kuna mpasuko mkubwa miongoni mwa vyama vya siasa juu ya jina la mgombea.

Hata hivyo, kuna juhudi kubwa zinafanyika ndani ya chombo hicho kuwadhibiti wabunge wake.

Mchakato wa wiki nzima wa kumtafuta mrithi wa Sergio Mattarela, ambaye muhula wake unamalizika Februari 3, mwaka huu, umefichua udhaifu wa siasa za Italia na kushindwa kwa uongozi katika muungano wa vyama vya mrengo wa kati wa kulia na kushoto.

Wakuu wa vyama vya League Party na kile cha Vuguvugu la Nyota 5, walisema kwa mara ya kwanza wanamtaka mwanamke kuwa rais na kuashiria uwezekano wa kuafikiana juu ya hilo.

Vyanzo tofauti vinasema vyama vyote viwili vinamuunga mkono Elisabetta Belloni, anayeongoza idara ya usalama wa taifa lakini bado anakabiliwa na upinzani kutoka vyama vingine.

# Asilimia 40 ya Watigray wanakabiliwa na njaa

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

SHIRIKA la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), limesema takriban asilimia 40 ya watu wa jimbo la Tigray, Kaskazini mwa Ethiopia wanakabiliwa na uhaba wa chakula.

Kwa mujibu wa ripoti ya shirika hilo hali ya maafa katika jimbo la Tigray ilianza baada ya mashirika ya misaada kulazimika kupunguza kazi zao kutokana na ukosefu wa petroli na mahitaji mengine ya ugavi.

Wafanyakazi wa mashirika ya misaada wanalazimika kutembea kwa miguu ili kwenda kutoa misaada.

Shirika la WFP limesema mapigano mapya pia yamesababisha njia za kupelekea misaada zipungue.

Tathmini ya Umoja wa Mataifa ilibainisha kwamba watu milioni 4.6 wanaowakilisha asilimia 83 kwenye jimbo la Tigray hawana uhakika wa kupata chakula na watu wapatao milioni mbili, kati ya hao wamo katika hatari kubwa zaidi ya kukumbwa na baa la njaa.

Mkurugenzi wa WFP Kanda ya Afrika Mashariki, Michael Dunford, alitoa tahadhari kuhusu kuongezeka kwa njaa katika mikoa jirani ya Amhara na Afar, ambayo alisema imeathiriwa na mapigano katika miezi ya hivi karibuni.

Dunford alisema shirika la WFP linafanya kila linalowezekana kuhakikisha misafara yake ya chakula na dawa inafika kwenye maeneo yaliyomo kwenye hali ngumu kutokana na mapigano.

Mkurugenzi wa WFP alisema pande zote katika mgogoro huo zinahitaji kukubaliana na kusitisha mapigano ili misaada na mahitaji mengine iweze kuwafikia watu wanaokumbwa na njaa.

**Habari zote na DW**

## MAKALA

# MATOKEO YA MITIHANI HAYAPIMI UKUAJI WA KIWANGO CHA ELIMU



Na Magabilo Masambu

KATIKA mifumo ya elimu duniani si Tanzania tu zinatumika njia mbalimbali za kupima maarifa yanayotolewa. Njia mojawapo ni kutumia mitihani ambayo hufanyika nyakati tofauti. Kuna mitihani inafanyika kabla ya kuanza kozi, katikati na mwishoni mwa kozi.

Unapimwa mwanzoni kufahamu unajua nini kabla ya kuanza kozi, unapimwa katikati kupata maendeleo ya mafunzo na unapimwa mwishoni mwa kozi ili kupata cheti ambacho ama kitakuonyesha umefuzu na kufaulu au umefuzu kwa kushindwa. Hiyo ni njia inayotumika kujaribu kuleta usawa hasa wakati wa ajira kwamba sifa itakuwa vile vyeti si mtu.

Mitihani hii mara nyingi inagawanyika katika sehemu kuu mbili, yaani ya nadharia au ya vitendo. Hapa kwetu tunayo baadhi ya masomo yanayofanyika kwa nadharia na vitendo kwa maana ya masomo ya sayansi na upande wa pili masomo kwa nadharia tu kwa maana ya masomo ya sanaa.

Swali hapa je, matokeo ya mitihani ya kitaifa hasa kidato cha pili, cha nne na cha sita yanaweza kuakisi ukuaji wa kiwango cha elimu nchini? Wanafunzi wakifaulu zaidi tunaweza kusema kiwango cha elimu kinapanda? Au wakifeli tunaweza kusema kiwango kimeshuka? Au ni mambo gani yanaweza kuonyesha kama tunapanda au tunashuka?

Kwa maoni yangu ni lazima kufahamu tofauti iliyopo kati ya kufaulu mitihani na upokeaji wa maarifa katika elimu yenyewe. Mfumo wetu wa elimu unamhitaji mwanafunzi akariri zaidi ili afaulu mitihani kuliko kumfanya apate maarifa. Hii ni kwa sababu pamoja na malengo mengine elimu yetu ina kusudia watu kupata vyeti. Ndiyo maana anayepata F kwenye masomo mfumo unamtafsiri kama hajui kitu na yule aliyepata alama A,B,C na D anatafsiriwa kama ndiye anayejua zaidi na anajivunia matokeo hayo kwa kujiona ana akili zaidi kuliko walioshindwa.

Lakini ukweli ni kwamba kama unataka kupima ukuaji wa kiwango cha elimu, unatazama matokeo ya kazi ambazo zinafanywa na wale waliokwisha kupata elimu hiyo. Maana yangu ni kwamba kama una maprofesa katika nchi wameisaidiaje nchi kutumia elimu waliyoipata? Kama una wahandisi wanaweza kufanya kazi bila usimamizi wa Wachina au wazungu?

Je uwezo wa kufikiri wa watu wako juu ya haki zao na mambo mengine yanayowahusu ukoje unakua au unarudi chini? Elimu imekupa wanasiasa wa aina gani, wenye fikra za namna gani juu ya nchi yao? Je, elimu hiyo imewezesha watu wengi kujitegemea zaidi au kadri wanavyosoma ndivyo wanavyokuwa tegemezi zaidi? Je, tumeitumia elimu kutengeneza wenyewe vitu ambavyo ni mahitaji ya watu wetu? Waliopata elimu uwezo wao wa kujieleza na kutenda ukoje? Je, kiwango cha watu wanaojua kusoma na kuandika kwa ufasaha kikoje? Haya ni machache tu kati ya mengi ambayo yanapaswa kutazamwa.

Ukishayatazama yote hayo ukajiridhisha kwamba viwango vyake vinaongezeka pamoja na vigezo vingine hapo sasa unaweza kusema kiwango cha elimu yetu kinapanda. Lakini yakiwa kinyume, maana yake tunatakiwa kubadili aina ya mfumo wetu wa elimu ili kutuwezesha kuyapata hayo na mengine zaidi.

Kwa sasa elimu yetu imejikita katika kutafuta matokeo mazuri ya mitihani na si kutoa maarifa yenye tija kwa wananchi na taifa, tuko kwenye kushindana nani anapata alama A zaidi na kupambana kufuta ufaulu wa alama F nadhani tungepambana zaidi kuhakikisha hata atakayepata F anapomaliza basi ile miaka minne aliyosoma iwe imemwezesha kufanya jambo kwa ajili ya maisha yake.

Hapa kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu lile kundi kubwa la wanafunzi ambao huwa hawaendelei na masomo kwamba huwa wanafanya kazi gani baada ya masomo ya darasani kuwashinda. Tukishafahamu shughuli zao basi zinaingizwa kwenye mtaala na tutakuwa tumepunguza watu watakaokuwa wanailalamikia serikali kuhusu ajira kwa sababu tayari elimu ya shughuli zao watakuwa wameshaipata.

Mfano kama tunadhani huwa wanafanya kilimo, ufugaji, biashara, uvuvi, ususi, ufundi au ujenzi basi hayo masomo yaingizwe kwenye mtaala na yafundishwe zaidi na upimaji wake uwe tofauti na huu wa mitihani kama unaofanyika sasa.

Najua mwanzo ni mgumu lakini inawezekana na walimu hawahitajiki waliomaliza digirii na ndilo tatizo letu lingine. Unakuta mtu ni mtaalamu kweli wa kufundisha jambo fulani, lakini tunataka awe na vyeti vya chuo kikuu. Hii ni kwa sababu elimu yetu ni ya vyeti ndiyo maana tunao watu wengi wenye vyeti lakini wajinga katika fani zao.

Tukishapata watu wanaozijua kazi kutokana na elimu au maarifa waliyoyapata na wakatenda bila utegemezi wa kusubiri wapewe ajira, ndipo tutajitapa kwamba kiwango cha elimu yetu kimekua.

Hatuna budi kutoka huko kwenye kushindana kupata alama za matokeo mazuri ya mitihani ya kitaifa pekee na kibaya zaidi tunashindanisha shule ambazo mazingira yake yako tofauti kuanzia miundombinu mpaka huduma. Walio kwenye mazingira ya yasiyoridhisha wanajiona wanyonge wanaposikia wenzao darasa zima limepata ufaulu wa daraja la kwanza na kisaikolojia wanaathirika na kujiona wametengwa.

Ushindani huu ndio unafanya mpaka wengine wanafanya udanganyifu kwenye mitihani ili wapate sifa ya kwamba wanafanya vizuri. Baadhi ya shule sasa zimekuwa na mtindo wa kuwachuja wanafunzi na kuwakataa wale wasiofanya vizuri. Je, huu si ubaguzi na tunakwenda wapi kama taifa? Hao wanafunzi wanaotengwa wanajisikiaje?

Kuna baadhi ya shule kama unataka kuhamia, wanataka matokeo yako kwanza na ikiwa huna alama wanazozitaka huwezi kukanyaga hapo halafu matokeo ya kitaifa wanajisifu kwamba wanafanya kazi kumbe wanafundisha wanafunzi wenye uwezo pekee.

Wizara yenye dhamana ya elimu itafakari zaidi hali ya elimu yetu. Hakuna haja ya kupambana watu wafaulu mpaka vyuo vikuu lakini wakishamaliza hawawezi kujitegemea. Elimu si msahafu kwamba kwa sababu wazungu walituachia Historia, Jiografia, Kiingereza na miongozo yake kwamba hatuwezi kubadili. Tubadili ili maarifa yawafae Watanzania wenye uwezo mkubwa wa akili na mdogo vile vile.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Rangi ya Chungwa' uliorekebishwa maneno studio



Na Adam Fungamwango

WIKI iliyopita kwenye safu hii tuliona baadhi ya nyimbo ambazo zilikataliwa kurekodiwa kwenye studio za Redio Tanzania Dar es Salaam kwa sababu mbalimbali.

Kifupi tu ni kwamba nilisema, Redio Tanzania au RTD kama ilivyokuwa inajulikana, kwa sasa ni TBC, ilikuwa na kamati iliyokuwa inapitia maneno ya nyimbo zote ambazo zilipelekwa kwa ajili ya kurekodiwa.

Kabla ya kurekodi, bendi zililazimika kupeleka mashairi ya nyimbo zote na kamati inayapitia neno kwa neno. Huko ndiko baadhi ya maneno yanakatwa na kuambiwa watumie maneno ambayo kamati imependekeza au ambayo wanamuziki wenyewe wataona inafaa. Baada ya kurekebishwa bendi inakwenda kurekodi.

Lengo la kamati kuzipitia, kuzirekebisha, kuzikataa na hata kuzipiga marufuku baadhi ya nyimbo ni kutoifanya jamii ya Watanzania kupotoka, kutoka kwenye utamaduni wao halisi na kuiga ya wengine, kuwa na adabu na heshima, yaani mkubwa na mdogo kuheshimiana, kusimamia maadili ya kitaifa lakini pia kuwafanya kuwa wamoja, wenye amani, utulivu na mshikamano.

Tuliona wimbo kama 'Mambo Kwa Soksi' wa Super Matimila, ambao baadaye alikwenda kuurekodi nchini Kenya na mashabiki wa muziki wakawa wanao kwenye kanda zao za kaseti, lakini haupigwi RTD.

Nyimbo zingine ni 'Kanyaboya', 'Cha Mlevi Huliwa na Mgema', na 'Dalila' zote za Juwata Jazz, Msondo Ngoma kutokana na sababu nilizoeleza hapo juu kuhusu maadili ya jamii.

Orchestra Safari Sound 'Ndekule' wao walikataliwa kurekodi nyimbo za 'Jabali', ulioimbwa kwa kiasi kikubwa na Muhidini Gurumo, na 'Nyama ya Nyani' uliotungwa na Molay Tunga ambaye baadaye mashabiki walimpachika jina la Nyama ya Nyani kutokana na wimbo huo ambao pamoja na kukataliwa kurekodiwa RTD, lakini ulipendwa mno ukumbini.

Leo tutaziangalia nyimbo ambazo awali zilikuwa na maneno fulani, ambayo yalirekebishwa kabla ya kurekodiwa kwa amri ya kamati ya RTD.

Tunaanza na 'Rangi ya Chungwa' uliopigwa na Nyanyembe Jazz Band. Ni wimbo maarufu uliopigwa takriban miaka 50 iliyopita. Leo hii hadi watoto wadogo wanaufahamu. Wengi hawajui kuwa wimbo huu wakati unarekodiwa haukuwa unaitwa hivyo bali 'Rangi ya Fanta'. Wakati wa unarekodiwa, waliulizwa kama wameingia mkataba wa kibiashara au wamelipwa kutangaza, wakasema hapana. Ndipo wakashauriwa waondoe neno Fanta, wakashauriwa waweke chungwa kwa sababu ni vitu vinavyofanana. Kutokana na hali hiyo, sehemu zote ambazo ziliimbwa neno Fanta ziliondolewa na kuwa chungwa.

Orchestra Makassy, walikuwa na wimbo wao unaitwa 'Asumani'. Kuna kipande kinaimbwa 'kila apitaye Asumani asabahi.' Awali kiliimbwa 'kila apitaye Athumani aopoa'. Jamaa wa kamati wakawaambia wachomoe neno kuopoa, kwa sababu si kiswahili sanifu, ila ni cha mtaani, ndipo likawekwa neno 'asabahi.'

Hata hivyo baadaye wimbo huo ulikwenda kurekodiwa nchini Kenya, neno 'aopoa' likawekwa kama kawaida. Kwa hiyo kuna ule uliorekodiwa Tanzania na ule uliorekodiwa Kenya na hata ukizisikiliza zinatofautiana kwa sababu wa Kenya, Dr. Remmy alikuwa ameondoka Makassy.

Wimbo wa DDC Mlimani Park Orchestra unaitwa 'Neema', nao ulichomolewa baadhi ya maneno pale kwenye sehemu inayoimbwa 'sina neno mimi kwa kuwa najua huyo ni mzazi mwenzio penzi maua.'

Kabla ya hapo kipande hicho kiliimbwa 'sina neno mimi kwa kuwa najua, kimada hana talaka, penzi maua.' Kamati ikapendekeza maneno hayo yachomolewe kwa sababu yana ukakasi ndipo yakawekwa 'huyu ni mzazi mwenzio.'

'Kipini cha Dhahabu' ni wimbo uliopigwa na bendi ya Biashara Jazz Band chini ya marehemu Juma Ubao. Kuna maneno yanasema 'nywele za bandia na kanga za mpunga wa kisele, sijui ni mtu gani anayemdanganya'. Hayo yaliwekwa baada kukataliwa kuimba hivi "nywele za bandia na kanga za Mombasa, sijui ni mtu gani anayemndanganya'. RTD wakawaambia waondoe neno kanga za Mombasa kwa sababu ni kuwatangazia biashara Wakenya wakati na sisi Tanzania tuna viwanda vyetu na kanga zetu. Wakati huo kanga za mpunga wa kisele zilikuwa kwenye chati sana. Wakachomeka neno hilo.

Juwata Jazz Band, wana wimbo unaitwa 'Mahmoud'. Kuna sehemu inaimbwa 'Wasiliana nami kesho Keko Machungwa.' Ililazimika iwe hivyo baada ya kukataliwa kuimba 'Wasiliana nami kesho, Polisi Ufundi'. Polisi Ufundi ndiyo kule kule Keko Machungwa. Kamati haikuona busara, wimbo wa mapenzi kuonyesha wapenzi hao wamekutania eneo la polisi. Kwa sababu eneo hilo pia linaitwa Keko Machungwa, wakashauri kuwekwa jina hilo, badala ya kutaja polisi kwenye wimbo wa mapenzi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-15

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

We mama Bupe, unaitwa huku."

Alikuwa ndani akiwa anatega sikio. Ujio wa mgeni huyo ulimtisha sana mama huyo, hivyo alisikia kila kitu kilichokuwa kikiongelewa. Maswali na majibu yote yaliingia masikioni mwake.

Wito ule ulimshtua zaidi ya kile kilichomshtua mwanzo. Aliitikia, lakini sauti haikutoka kwa woga.

Alijikuta akitoka nje, akiwa anajivuta kama mbuzi anayekwenda machinjoni.

"Huyu ndiye aliyenikaribisha. Ahsante sana mama, nitakuja siku nyingine." Alisema naye akimfuata na kumpa noti iliyobaki mkononi mwake ya shilingi elfu kumi.

Woga na mshangao alioupata mama Bupe alishindwa hata kuipokea pesa hiyo, na badala yake mikono yake ikashindwa kufanya kazi kutokana na ganzi, ikaanguka chini na kuanza kupeperuka na upepo.

Haraka mzee, Kalango alifanikiwa kuiokota.

"Nipe hela yangu." Mama Bupe alimwambia mumewe.

"Unapokea pesa kizembezembe, nitaichukua mimi na hii."

Eddy aliangua kicheko dhaifu na kusema " Hapana mzee mpe mama, alikosea tu kuipokea."

Mzee Kalango kidogo imani ilimrudia. Aliona askari huyo hakuja kwa nia mbaya. Na kwa bahati nzuri na yeye aliamua kuongea kila kitu ukweli kama ulivyo.


****************************

Aliamka akiwa mchovu. Lakini haikumfanya ashindwe kuunyoosha mkono wake na kuchukua simu yake ya mkononi.

Mara nyingi huwa anaizima. Wakati wa kulala huwa hataki bughudha na mtu. Kila kitu kizuri au kibaya huwa anakishtukia asubuhi akiwa amefungua simu. Na hii huifanya sana akiwa hayupo kwenye operesheni yoyote ya kutisha au hajakesha kwenye starehe au kazi zake.

Alipoiwasha tu, akaona kuna meseji imeingia. Akaifungua na kuisoma. Akatabasamu. "Mwanamke huyu!" alijiambia mwenyewe. "Mwenye simu hii mzima kweli?" Ndivyo ilivyoandikwa.

Kwa muda wa miezi mitatu ambayo Eddy ameishi na Mwahija kama mpenzi wake alikuwa amembadilisha kwa kiasi kikubwa.




**Alipoiwasha tu, akaona kuna meseji imeingia. Akaifungua na kuisoma. Akatabasamu. "Mwanamke huyu!" alijiambia mwenyewe. "Mwenye simu hii mzima kweli?" Ndivyo ilivyoandikwa. Kwa muda wa miezi mitatu ambayo Eddy ameishi na Mwahija kama mpenzi wake alikuwa amembadilisha kwa kiasi kikubwa.**

Kwa kawaida Eddy Kamal, ni pamoja na kazi yake ya upelelezi, lakini ni mtu mkarimu, mcheshi na mizaha mingi.

Hii ilimfanya si tu kupata marafiki wengi, ambao wengi hawakuifahamu kazi yake, lakini pia kupata wasichana wengi. Hakuona hata mmoja wao ambaye roho yake imeridhika naye, ingawa kwa Mwahija alionekana kama ameanza kunasa.

Tabia ya Eddy ilionekana kumbadilisha Mwahija kwa kiasi kikubwa, kiasi kwamba akawa naye anaiga baadhi ya mizaha ya mpenzi wake ambapo awali hakudhania kama anaweza kuwa mtu wa aina hiyo.

"Aaa Wapi?" Aliandika meseji na kuituma. Sekunde chache baadaye ikaja nyingine. "Kafanyaje tena?" Iliandikwa.

"Kalala kaniachia simu." Aliandika na kuituma. Haikupita hata nusu dakika simu ikapigwa. Akaipokea.

"Unanirusha roho ee, yaani ningesikia sauti ya kike, ningekuja huko huko Kijitonyama." Ilikuwa ni sauti ya Mwahija ambayo mbali na kwamba alionekana kuzunguza kimzaha, lakini ilikuwa anamaanisha. "Kwani wewe ulidhani ni nani anajibu meseji, wakati simu yangu?""Hiyo meseji ya mwisho ndiyo imenishtua, kalala kaniachia simu, wee."

"Ukajua ni kweli."

"Abiria chunga mzigo wako baba."

"Unachunga mzigo uko Kijitonyama, wenyewe uko Tegeta, unachunga vipi hapo mzee mwenzangu?"

"Unadhani kuchunga mtu ni kama unachunga ng'ombe? Tunakumbushana tu ili kila mmoja asisahau wajibu wake kwa mwenzake mzee." Ni jibu ambalo lilimfanya Eddy acheke.

"Mwahija nikwambie kitu kimoja tu, mimi ni wako na hakuna mwingine."

"Una uhakika mzee mwenzangu?" Swali hilo jinsi lilivyoulizwa na aina ya maneno yenye pia lilimfanya Eddy azidi kuvunjika mbavu.

"Siku hizi unakula nini wewe, mbona umekuwa na tabia ya kunivunja mbavu tu?" "Si umenifundisha mwenyewe maneno yako ya mizaha, sasa karibu nikuzidi wewe mwalimu wangu."

"Okay, hebu tuongee maneno ya maana sasa, wiki nzima hatujaonana sasa, najua wote tuko bize, lini tuonane?" Aliuliza Eddy.

"Leo si Jumapili? Jumatano mimi nakuja kwako nikitoka kazini."

"Okay sawa, ile kazi niliyokutuma ukaikamilisha, nimeshaifanya." "Ipi?"

"Ya yule mzee Kalango."

"Mmmh, wewe tena, usifike?"

"Nashukuru kwa msaada wako mpenzi, nimepata nilichokuwa nahitaji."

"Na mimi pia nimefanya kwa sababu yako Danny, nakupenda sana."

Ahsante sana, kwangu mimi ni kwamba hakuna neno la Kiswahili linaloonyesha kuwa unampenda mtu kuliko kawaida, zaidi ya neno lile lile moja tu, nakupenda." Ilikuwa zamu ya Mwahija kucheka. Alicheka kwa mawili. Moja jinsi Eddy alivyotumia sanaa kwenye maneno hayo, pili ile kuambiwa anapendwa tu kwake ilikuwa furaha tosha.

Baada ya kukata simu alikumbuka jana yake alikuwa Mbagala Charambe. Alikutana na aliyekuwa hausiboi wa nyumba ya marehemu Chilambo. Alifuata ramani yote aliyoelekezwa ingawa alikwenda na gari. Alimkuta kwa rafiki zake anacheza drafti. Kwanza alishtuka, lakini alimtuliza na hakutaka tena kujitambulisha kuwa ni askari polisi. Alimdanyanya kama alivyomdanganya Mwahija. Yeye ni Mjomba wa Tina. Alitaka apate taarifa zote za ndani jinsi walivyokuwa wanaishi na ni kitu gani kilitokea siku ya tukio mpaka Tina akakasirika akafanya jambo lile. Shilingi elfu hamsini ilimfanya Hussein kufunguka anachokifahamu kuhusu nyumba ile na mpaka siku Tina anakamatwa.

Vyote alivyopata kwa mzee Kalango na Hussein, alidhani tayari vilikuwa vinatosha kwa kuanzia juu ya kuirudisha upya kesi ya mauaji ambayo Tina anatuhumiwa kumuua bosi wake Chilambo. Alichukua tena simu yake ya kumpigia rafiki yake wakili Florence Tinga. "Niambie Eddy." "Poa tu, mambo vipi?

"Safi, umenipigia asubuhi hii nadhani kutakuwa na jambo."

"Jambo lipo, ila tukutane ofisini kwangu saa sita mchana leo."

"Vipi, hebu nipe muktasari Eddy ni jambo gani hilo?" "Nina mzigo wako."

"Nadhani itakuwa ni ile ya yule msichana, ndiyo?" "Uko sahihi."

"Umekamilisha kila kitu?" "Siwezi kusema kila kitu, ila nadhani kuna vitu ambavyo vitatusaidia."

"Okay, nakuja."

Wakati huo alimwita Tinga akijua kesho yake ana kibarua kingine cha kwenda kwenye hoteli ya Moon Light, Sinza Dar es Salaam.

Ilikuwa ni moja kati ya eneo ambalo alitakiwa kwenda kukamilisha uchunguzi, kwani baada ya kuwahoji wote wawili, mzee Kalango na Hussein, aliona upelelezi wake hautotimia mpaka afike kwenye hoteli hiyo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# SERIKALI KURUDISHA TUZO ZA WANAMUZIKI

HATIMAYE serikali imerudisha tena tuzo za wasanii wa muziki nchini zinazojulikana kama 'Tanzania Music Awards' ambazo zitatolewa Machi 26, mwaka huu.

Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, amesema hayo wakati akitoa tuzo kwa wasanii wa muziki walionufaika na tozo za mirabaha mwaka 2021.

Mchengerwa amesema utekelezaji wa maelekezo hayo unatokana na ahadi ya Rais Samia kuhusu wasanii kunufaika kwa kazi kupata tuzo na mirabaha ya kazi zao.

"Nawaagiza makatibu kuhusu kuandaa mashindano ya Afrima na BET, kuandaliwa hapa nchini, kujipanga ili kuanza kufanyika tuzo hizo hapa nchini," amesema Waziri Mchengerwa.

Tuzo hizo zilienda sambamba na kuwakabidhi hundi za pesa zilizotokana na mirabaha iliyotolewa na Taasisi ya Hatimiliki Tanzania (COSOTA) iliyofanyika juzi katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere.

Mirabaha hiyo imetokana na kazi zao kuchezwa katika vyombo vya redio vya EFM, TBC Taifa, TBC FM, Arusha na Pangani kutoka Tanga.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas amesema mirabaha hiyo inatolewa kwa wasanii ambao nyimbo zao zilichezwa katika vyombo mbalimbali vya redio.

Kaimu Mtendaji wa BASATA, Matiko Mniko amesema tuzo hizo zinalenga kutambua mchango unaotolewa na wasanii, wadau na vikundi vinavyofanya kazi hapa nchini.

# Burudani moja ya chanzo cha unyanyasaji watoto

**Rausath Sued na Milembe Mipawa,** SJMC

TASNIA ya burudani ni moja ya eneo linaloonekana kutotizamwa kikamilifu na kusababisha kuwepo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Sheria ya mtoto ya mwaka 2009, ibara ya 4 kifungu (1) inasema mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 hujulikana kama mtoto. Malezi kwa mtoto imekua ni gumzo kubwa katika jamii, kwani baadhi ya wazazi wameonekana kutoa malezi kinyume na mila na desturi za jamii.

Katika mitandao ya kijamii watoto wanaonekana wakitumika kutoa burudani aidha kwa kupenda au kutokupenda, ambapo swala hilo ni kinyume na malezi, kwani mtoto ana haki ya kulindwa.

Nchini Tanzania kumekua na matukio yanayohusisha wazazi kuwa waamuzi wa kila kitu kwa watoto wao hususani katika mitandao ya kijamii iliyofungamana na burudani, vitendo hivi vimeshamiri kwa wingi nchini. Consolatha Maganga anasema mtoto wake ameamua kumuweka katika mitandao ya kijamii na kumuhusisha na burudani ili kukuza kipaji chake na amuandae awe mwenye kujiamini.



Mbali na baadhi ya wazazi kumuandalia ujasiri mtoto katika mitandao ya kijamii, Abdallah Mpwani anapingana na kauli hiyo kwa kusema ni bora kumlea kwa makuzi ya kawaida kuliko kuendeshwa na utandawazi kwa maendeleo yake ya baadae.

Theresia Kinabo wakili wa kujitegemea wa shirika moja la haki za binadamu, anasema kitendo cha baadhi ya wazazi kuwageuza watoto kuwa chanzo cha kujipatia kipato kwa njia ya burudani katika mitandao ya kijamii, ni ukatili pia ni kinyume na sheria.

Kwa mujibu wa taasisi isiyo ya kiserikali ya C-SEMA, inaeleza mtoto akiwa salama dhidi ya vitendo vya unyanyasaji kuna uwezekano mkubwa wa kukua na kuendelea vizuri.

# Baba levo apewa dili jingine

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva nchini, Revokatus Kando, 'Baba levo' amempongeza Mtangazaji Mwijaku kwa kupongezwa na Rais Samia Suluhu kwa kuthubutu kugombea nafasi ya Uspika.

Akizungumza wakati alipokuwa amepata dili la ubalozi wa The African Princess Casino kwa miezi sita Baba Levo, amesema kuwa anampongeza Mwijaku kwa kupongezwa na Rais lakini isiwe shida sasa.

"Nimepata Ubalozi wa miezi sita African Princess Casino nitatoa nafasi ya wasanii wenzangu kupata ajira na kuweza kufanyakazi zao." alisema

Aidha amesema kuwa mtonyo anaolipwa kupitia ubalozi huo unaingia mara 100 mshahara wa mtangazaji mwenzie Mwijaku akitamba hawezi kujifananisha nae.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### AUBAMEYANG AWANIWA BARCA

BARCELONA na Juventus wamewasilisha ombi rasmi la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 32 kwa mkopo kwa kipindi cha msimu kilichosalia. ***(Athletic)***

#### RAPHINA ATAKIWA WEST HAM

KOCHA wa West Ham, David Moyes anafikiria kumsajili mshambuliaji wa Leeds United, Raphina na ana mpango wa kumnunua kabla ya dirisha la uhamisho la Januari kufungwa. ***(Mirror)***

#### STERLING BADO

WINGA wa England, Raheem Sterling anatarajiwa kuendelea na mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na Manchester City. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 unamalizika mwaka 2023 na Barcelona PSG na Real Madrid zina nia ya kumsajili. ***(ESPN)***

#### BURN AWINDWA

NEWCASTLE United inatarajiwa kuimarisha ombi lao la kumsajili beki wa Brighton mwenye umri wa miaka 29, Dan Burn na pia wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketia mwenye umri wa miaka 22. Mkataba wa sasa wa Nketia unakamilika msimu ujao. ***(Guardian)***

#### ERIKSEN KUSAINI

KLABU ya Brentford inatumaini itaweza kutangaza usajili wa mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen wikiendi hii. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 aliwekwa kidhibiti moyo bada ya kuzimia wakati wa michezo ya Euro 2020 Juni. ***(Times)***

#### RAMSEY KUBAKI

NYOTA wa Wales, Aaron Ramsey huenda akabakia katika klabu ya Juventus baada ya kukataa uhamisho wa kuelekea Aston Villa, Burnley, Crystal Palace, Newcastle United na Wolves mwezi huu. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

#### LOFTUS NA EVERTON

KLABU ya Everton ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Ruben Loftus Cheek kutoka Chelsea. ***(Mail)***

#### EKITIKE AGOMBEWA

WEST Ham ipo katika mazungumzo na klabu ya Reims kuhusu mkataba na mchezaji mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ufaransa, Ekitike, ambaye pia amehusishwa na uhamisho wa Brentford, Brighton na Newcastle United. ***(Sky Sports)***

#### VILLA WAKATALIWA

DAU la Aston Villa la pauni milioni 20.8 kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Uruguay, Rodrigo Bentancur limekataliwa na Juventus. ***(Guardian)***

#### SPURS WAGOMEWA

TOTTENHAM Hotspur pia inataka kumsajili, Rodrigo Bentancur lakini wanataka kumnunua kwa mkopo ombi ambalo Juventus haijalikubali. (***Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA
### MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD APEWA OFA YA UKOCHA EVERTON

### ●●● Ni baada ya Wayne Rooney kuipiga chini nafasi hiyo akitaka kuendelea kuinoa Derby huku...

**LIVERPOOL,** England

EVERTON imeripotiwa kumpa ofa Frank Lampard ya kuwa kocha mpya wa klabu hiyo baada ya mchezaji wao wa zamani, Wayne Rooney kuikataa nafasi hiyo.

**Lampard mwenye umri wa miaka 43, amekuwa hana kazi tangu alipofukuzwa na Chelsea, Januari mwaka jana.**

Everton imekuwa ikitafuta kocha mpya tangu ilipoachana na Rafael Benitez mapema mwezi huu.

Raia huyo wa Hispania alishinda mechi tatu kati ya nne za kwanza, lakini moja tu kati ya 13 zilizopita hapo Goodison Park kabla ya kufukuzwa.

Awali Toffees hao walimtaka Rooney, lakini ikaripotiwa kwamba aliikataa nafasi hiyo na kuamua kubakia na timu inayosuasua kwenye Championship, Derby.

Akizungumza mapema Ijumaa, Rooney alisema: "Everton wamewasiliana na wakala wangu na kumuomba nifanye nao mahojiano kuhusu kazi, lakini nilikataa.

"Yalikuwa maamuzi magumu. Naamini nitakuwa kocha kwenye Ligi Kuu na nipo tayari kwa asilimia 100%.

"Kama hiyo itakuja kwa Everton, itakuwa vizuri. Lakini kwa sasa nina kazi na Derby, ambayo ni muhimu kwangu."

Vitor Pereira, ambaye alifukuzwa na Fenerbahce Desemba, alionekana kuwa ndiye anayeongoza kwenye nafasi hiyo. Hata hivyo, mmiliki wa Everton, Farhad Moshiri alibadili mawazo baada ya mashabiki wenye hasira kulikataa jina hilo.

Pereira mwenye umri wa miaka 53, pia amewahi kuzinoa Porto, 1860 Munich na Olympiacos.

Lampard aliifikisha Chelsea nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu na alitinga fainali ya FA katika msimu wake mmoja pekee.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

EGYPT
VERSUS
MOROCCO

1 | 3.37
X | 2.78
2 | 2.42

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCA YAKARIBIA KUMNASA MORATA



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inajiamini kwamba ina uhakika kumsajili Alvaro Morata mwezi huu, vyanzo vimeitonya 90min, huku nyota wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang pia akiwemo kwenye orodha.

Fowadi huyo kwa sasa anacheza kwa mkopo pale Juventus akitokea Atletico Madrid na amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Barca kwa muda mrefu.

Mwanzoni mwa dirisha hili dogo la usajili ilionekana wazi kuwa anaweza kutua klabuni hapo, lakini mambo yalishindikana.

Hata hivyo, 90min inaelewa kwamba Barcelona haijakata tamaa ya kumsajili mchezaji huyo katika dirisha hili la Januari hii ambapo linafungwa kesho.

Xavi anatajwa kwamba ni shabiki mkubwa wa mshambuliaji huyo na anafanya kila analoweza kumpeleka pale Blaugrana.



# Vlahovic rasmi asajiliwa Juventu

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imekamilisha usajili wa Dusan Vlahovic kutoka Fiorentina kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 70.

Straika huyo ambaye alifikisha umri wa miaka 22 Ijumaa, amekubali kusaini mkataba wa miaka minne na Bianconeri hao baada ya kufuzu vipimo vya afya yake.

Juve italipa ada ya euro milioni 70 kwa awamu kwa kipindi cha miaka mitatu, pamoja na gharama ya ziada euro milioni 11.6.

Vlahovic msimu huu anao za kwa kufunga mabao kwe Ligi Kuu ya Italia, Serie A al nayo 17 kutoka mechi 21 saw nyota wa Lazio, Ciro Immob

Alikuwa akihusishwa na bu nyingi kubwa barani U baada ya kuonesha kiwango kuvutia kwa kipindi cha mis miwili.

Vlahovic amejiunga na I similiano Allegri hapo J ambayo mara zote imek kwenye wakati mgumu wa funga mabao msimu huu, w wa wamefunga mabao 34 ka mechi 23 za Serie A.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# COASTAL YAKANUSHA KUMTIMUA KOCHA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umekanusha taarifa za kumtimua Kocha wake Mkuu, Melis Medo huku akitajwa kurejeshwa Juma Mgunda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno alisema hakuna ukweli juu ya taarifa ya kumtimua kocha wao Melis kwa sababu ya matokeo mabaya waliyoyapata katika mechi za hivi karibuni.

Alisema hakuna ukweli wa hilo jambo na kwamba ni uzushi wa watu wachache ,bado wapo na kocha huyo na wanamsapoti katika kazi zake kuhakikisha timu yao inapata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

**“Bado tupo na Melis Medo na tunashirikiana halafu tuna mkataba nae wa miaka miwili, hatuwezi kumudu fedha za kuvunja hata mkataba wake labda yeye mwenyewe atake kujiuzulu,” alisema Mgweno.**

Aliongeza kuna uzushi wa watu wachache wanaosambaza maneno hayo, na ana imani kocha huyo ataendele kuinoa timu hiyo hadi mkataba wake utakapofikia tamati.

“Msimu huu hatukuwa vizuri na kikosi kimekuwa na mabadiliko makubwa kiuchezaji na hata kupata matokeo mazuri, tukimuacha Medo kila mtu atatushangaa,” alisema.

Coastal Union ipo nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa imecheza michezo 13, ikishinda minne, kutoka sare tano na kupoteza mitano na imejikusanya pointi 17.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa na Naibu wake, Pauline Gekul wakipokea tuzo ya shukrani kutoka kwa watendaji wa Wizara hiyo kwa mchango wao kwenye sekta ya sanaa Januari 28, 2022 jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOHN MAPEPELE**

# *Simba Queen haishikiki, Opah hakamatiki*

**Na Adam Fungamwango**

NANI ataizuia Simba Queens? Hilo ni swali ambalo linaulizwa na mashabiki wa soka ya Ligi ya Wanawake nchini baada ya juzi, timu hiyo kuendeleza vipigo, kwa kuitwanga Mlandizi Queens mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, jijini Dar es Salaam.

Yalikuwa ni mabao ya Pambani Kuzoya na straika hatari wa timu hiyo, Opah Clement aliyefunga mabao mawili na kufikisha jumla ya mabao 15 aliyopachika msimu huu kwenye mechi nane tu alizocheza. Huenda msimu huu akawa mfungaji bora, baada ya msimu uliopita kunyang'anywa tonge mdomoni dakika za mwisho na Aisha Masaka wa Yanga Princess.

Ni ushindi wa nane mfululizo wa Simba Queens unaoifanya kuwa na asilimia 100 za ushindi, ikifikisha pointi 24 na mabao 45 ya kufungwa, ikifungwa mabao mawili, zaidi ya yote ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Mechi zingine zilizopigwa juzi ni kati ya Baobab Queens iliyokuwa nyumbani, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, ikiishindilia Alliance Girls ya Mwanza mabao 2-0 na kuifanya timu hiyo kuendelea kujikita kwenye nafasi ya pili kwa pointi 21 na kuikimbiza Simba Queens, ingawa yenyewe imefikisha mechi ya tisa, huku Simba Queens ikicheza nane tu.

JKT Queens ilikiona cha moto, ilipobabuliwa mabao 3-1 nyumbani kwenye Uwanja wa Meja Isamuhyo dhidi ya The Tigers Queens ya Arusha, huku Ruvuma Queens yenyewe ikipata ushindi nyumbani, Uwanja wa Majimaji Songea, dhidi ya Oysterbay Queens.

Pamoja na kufungwa, JKT Queens bado inashikilia nafasi ya tatu kwa pointi 14, huku Alliance Queens ikiwa nafasi ya nne kwa pointi 12, The Tigers Queens nafasi ya tano kwa pointi hizo hizo 12.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 30/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 4518 | VVV Venlo vs Dordrecht | 1.68 | 3.85 | 4.38 |
| 15:00 | 1439 | Puskas Akademia vs Videoton FC | 2.56 | 3.29 | 2.47 |
| 15:00 | 3049 | Chindia Targoviste vs CS Mioveni | 2.44 | 2.94 | 3.04 |
| 15:30 | 5968 | Union Saint Gilloise vs Anderlecht | 2.28 | 3.44 | 2.90 |
| 15:45 | 3606 | Rio Ave vs Varzim | 1.44 | 4.02 | 7.05 |
| 16:00 | 1532 | Panetolikos vs Aris Salonica | 3.31 | 3.06 | 2.24 |
| 16:00 | 2844 | Leganes vs Alcorcon | 1.74 | 3.48 | 4.61 |
| 16:00 | 5797 | Green Eagles vs Nkwazi | 1.74 | 3.27 | 4.53 |
| 16:15 | 4943 | Lausanne-Sport vs St. Gallen | 2.28 | 3.50 | 2.86 |
| 16:30 | 1235 | Vicenza vs Alessandria | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 16:30 | 1370 | Parma vs Crotone | 1.73 | 3.39 | 4.82 |
| 16:30 | 2728 | Almere City vs Telstar | 1.84 | 3.72 | 3.67 |
| 16:30 | 3683 | Cittadella vs Cosenza | 1.46 | 4.02 | 6.86 |
| 16:30 | 5720 | Derby vs Birmingham | 2.28 | 3.09 | 3.14 |
| 17:00 | 1858 | Lokomotiva Zagreb vs Hrvatski Dragovoljac | 1.23 | 5.40 | 9.63 |
| 17:00 | 4941 | GD Chaves vs CD Feirense | 2.14 | 3.27 | 3.22 |
| 17:15 | 2288 | Mezokovesdi SE vs MTK Budapest | 2.69 | 3.37 | 2.32 |
| 18:00 | 1872 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 1.84 | 3.59 | 3.94 |
| 18:00 | 2232 | Egypt vs Morocco | 3.37 | 2.78 | 2.42 |
| 18:00 | 5049 | RS Waasland Beveren vs KVC Westerlo | 3.47 | 3.76 | 1.88 |
| 18:00 | 5500 | U Craiova SA vs Argesul Pitesti | 2.70 | 2.80 | 2.84 |
| 18:00 | 5551 | FC Cartagena vs Fuenlabrada | 1.92 | 3.23 | 4.01 |
| 18:15 | 4521 | AEK Athens vs Volos | 1.32 | 5.12 | 8.26 |
| 18:30 | 1738 | Portimonense vs Tondela | 2.01 | 3.25 | 3.70 |
| 18:30 | 2313 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 18:30 | 2517 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 18:30 | 4170 | FC Luzern vs FC Basel | 3.06 | 3.65 | 2.11 |
| 18:45 | 4617 | ADO Den Haag vs De Graafschap | 2.75 | 3.38 | 2.35 |
| 19:00 | 1582 | Leones FC vs Universitario Popayan | 1.37 | 4.25 | 7.35 |
| 19:00 | 2778 | Cardiff vs Nottingham | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 19:30 | 3156 | Dinamo Zagreb vs HNK Rijeka | 1.28 | 5.00 | 8.46 |
| 20:00 | 3569 | Apollon Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.41 | 4.58 | 6.96 |
| 20:15 | 2188 | Mirandes vs Malaga | 2.18 | 3.15 | 3.29 |
| 20:30 | 2160 | Bergerac Perigord FC vs St Etienne | 5.73 | 4.35 | 1.49 |
| 20:30 | 3698 | Standard Liege vs Mechelen | 2.07 | 3.50 | 3.26 |
| 20:30 | 3866 | PAOK vs Olympiakos | 2.50 | 3.14 | 2.80 |
| 20:30 | 4023 | Academica vs Leixoes | 2.45 | 3.14 | 2.79 |
| 21:00 | 1545 | Hapoel Tel Aviv vs Hapoel Hadera | 1.95 | 3.24 | 3.58 |
| 21:00 | 2005 | Dinamo Bucuresti vs Steaua Bucuresti | 5.52 | 3.84 | 1.57 |
| 21:00 | 2533 | Sporting Braga vs Moreirense | 1.43 | 4.43 | 6.70 |
| 21:30 | 1734 | Maccabi Netanya vs Maccabi Haifa | 6.74 | 4.43 | 1.38 |
| 22:00 | 2636 | Patriotas FC vs Deportivo Pereira | 2.75 | 3.13 | 2.40 |
| 22:00 | 3764 | Senegal vs Equatorial Guinea | 1.56 | 3.42 | 7.34 |
| 22:00 | 4787 | Ujpest FC vs Ferencvaros TC | 5.39 | 4.24 | 1.47 |
| 23:00 | 1060 | Ponferradina vs Tenerife | 2.50 | 2.89 | 2.99 |
| 23:00 | 1968 | Real Santander vs Tigres FC (COL) | 1.50 | 3.81 | 5.79 |
| 23:00 | 5765 | Kortrijk vs Brugge | 4.53 | 3.94 | 1.67 |
| 23:00 | 5995 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 23:05 | 4893 | Canada vs USA | 2.63 | 3.06 | 2.54 |
| 23:30 | 1134 | Porto vs Maritimo | 1.12 | 7.49 | 19.70 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Januari 30, 2022
Nipashe



Lampard apewa ofa ya ukocha UKURASA 21

## Simba SC yaifungia kazi Dar City FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema ushindi ni silaha kubwa wanayoishikilia kwa sasa wakati leo wakishuka dimbani kuivaa Dar City kwenye mchezo wa kombe la FA raundi ya 32.

Kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi kitashuka kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa ili kujitafutia ushindi ili kiweze kutinga 16 bora ya mashindano hayo.

Ikumbukwe Simba ni mabingwa watetezi wa kombe hilo na waliweza kushinda katika fainali dhidi ya Yanga mwaka jana, mchezo uliopigwa uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Akizungumza kuelekea mchezo huo Kocha Pablo amesema wamefanya maandalizi ya kutosha na ana matarajio makubwa ya kupata matokeo chanya na kuweza kurudi katika ramani ya ushindi.

"Tumefanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika mechi za nyuma za kwenye Ligi, tunasahau matokeo hayo na sasa tunakwenda uwanja wa nyumbani kusaka ushindi dhidi ya Dar City ili kurejesha hali ya kujiamini kwa timu na wachezaji," alisema Pablo.

Alisema wana waheshimu wapinzani wao, kwani timu yeyote iliyoingia kwenye mashindano hayo ina nia ya kushinda na wanaamini watapa ushindani mkubwa.

"Tumejiandaa vizuri, tumewafuatilia wapinzani wetu kwa umakini na kuangalia madhaifu yao, na sasa kazi kubwa imebaki wachezaji kufanya majukumu yao ndani ya uwanja ikiwemo kusaka ushindi dhidi ya Dar City," aliongeza Pablo.

Simba inaingia kwenye mchezo huo ikiwa na kumbukumbu mbaya ikitoka kupoteza michezo miwili ya Ligi Kuu na mmoja wa sare.

Ilianza kwa kufungwa bao 1-0 na Mbeya City, halafu ikatoka sare na Mtibwa Sugar kabla ya kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Kagera Sugar.



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele akishangilia bao pekee alilofunga dhidi ya Mbao FC kwenye mchezo wa kombe la FA jana katika uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza. **PICHA: YANGA**

# Mayele aipeleka Yanga 16 bora

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Afunga bao safi la kichwa akiruka katikati ya mabeki wawili, huku Mbao ikitoa upinzani mkali..

STRAIKA hatari wa Yanga, Mkongomani Fiston Mayele, aliifungia timu yake bao pekee na kuipa ushindi wa 1-0 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza jana.

**Mayele alipachika bao hilo kwa kichwa dakika ya 52, baada ya krosi maridadi iliyochongwa na Farid Mussa.**

Akiwa katikati ya walinzi wawili, Hamisi Kasanga na Ruben Aloyce, Mayele aliwazidi ujanja na kupiga kichwa mpira na mpira ulimshinda golikipa, Wandwi Jackson na kujaa wavuni.

Ni ushindi ulioipeleka timu hiyo hatua ya 16 bora ya Kombe la FA linaloendelea wiki hii.

Haikuwa mechi rahisi kama ilivyotegemewa na mashabiki wengi, kwani ilibidi wanafainali hao wa msimu uliopita kupigana machozi, jasho na damu kupata ushindi kwa Mbao iliyo Ligi ya Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Mbao FC, ambayo ilionekana kama itapigwa bao nyingi, ilikuwa na wachezaji wengi chipukizi ukiondoa Robert Ndaki ambaye alikuwepo kwenye kikosi kilichocheza Ligi Kuu, kilitandaza kandanda safi, huenda kuliko baadhi ya timu za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa.

Wachezaji wengi walionekana kuwa na vipaji halisi vya mpira, wakipasiana bila woga, na kutoa ushindani wa kweli uliowashangaza wengi.

Iliangushwa na kukosekana kwa straika mmoja mwenye kuweza kufunga mabao tu.

Mbao ilifanya shambulio la kwanza kwenye lango la Yanga dakika ya 12, baada ya krosi ya mchezaji mkongwe Ndaki, kumkuta Shaaban Seif aliyeruka peke yake, lakini kichwa chake kikamlenga Kipa Aboutwalib Mshery, akaukamata mpira bila tabu yoyote.

Dakika ya 25 na 26, Jusue Moloko aliikosesha Yanga mabao, baada ya kuruka juu na kupiga kichwa mpira wa krosi wa Yassin Mustapha, lakini ukatoka nje kidogo, na dakika moja baadaye mpira alioupiga kichwa kutokana na kona, ulisababisha kizaaza langoni, ukagonga mwamba wa juu na kutoka nje.

Mayele nusura aifungie Yanga bao dakika ya 30, baada ya kuupata mpira akiwa karibu na lango akilipa mgongo lango la Mbao, lakini kama kawaida yake ni mwepesi, aligeuka ghafla na kuachia shuti lililopanguliwa na Kipa Wandwi Jackson na kuwa kona.

Wandwi tena alifanya kazi ya ziada dakika ya 45, alipopangua shuti la mbali na Dickson Job aliyeukuta mpira uliookolewa kizembe na mabeki wa Mbao.

Kipindi cha pili, baada ya mabadiliko ya hapa na pale kwa timu zote, ndipo Yanga ilipopata bao, ikiendelea kukosa mabao kupitia kwa Mustaha aliyepiga shuti kali dakika ya 56, lakini Wandwi alipangua kwa umaridadi, Nassor Aziz Bitebo, aliyeisumbua ngome ya Yanga, aliwatoka mabeki na kuingia ndani ya eneo la hatari, akaachia shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango dakika ya 76.

Chico Ushindi aliyeingia dakika 15 za mwisho, akichukua nafasi ya Ambundo, alipiga faulo iliyokwenda kugonga mwamba wa juu dakika ya 80.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9
9 770856 541002 >